
Nipashe
Jumatatu Agosti 24, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580318
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## JPM aendesha harambee kanisani kuchangia msikiti

UKURASA 2


22 Nipashe
HABARI MICHEZO
DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA
RONALDO KWA MBAPPE, AMKATAA NEYMAR REAL
Ni uwekezaji, litakuwa jambo la maana zaidi kumsajili mchezaji kijana kati yao hao...

UKURASA 22

# Mbivu, mbichi kujulikana wiki hii

• **Hatima** ya wagombea urais, ubunge, udiwani mikononi mwa NEC... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3
**TABOA YALIA UKATISHAJI TIKETI KWA MTANDAO**
CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), kimesema kuna...

UKURASA WA 4
**WAGOMBEA CCM, CUF, ACT WACHANGAMKIA FOMU**
WAGOMBEA ubunge kwa tiketi za CCM, ACT-Wazalendo na CUF jana...

UKURASA WA 5
**JUKATA KUJA NA SERA KUSHINIKIZA UTEUZI SAWA**
JUKWAA la Katiba Nchini (JUKATA), limeonyesha wasiwasi wake kwa...

## Mpina aanika mafanikio miaka 5

UKURASA 3



Rais John Magufuli akipokea michango kutoka kwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, Mhashamu Beatus Kinyaiya, kwa ajili ya ujenzi wa msikiti wa Chamwino, baada ya kuitisha harambee aliposhiriki Misa Takatifu ya Dominika ya 21 ya Mwaka "A", pia alizindua kanisa, nyumba ya mapadri na Grotto ya Parokia ya Bikira Maria Imakulata Ikulu Chamwino jana. **PICHA: IKULU**

Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

## Askofu Katoliki ataja sifa saba za uongozi

UKURASA 3

**MICHEZO** BWALYA, ONYANGO GUMZO SIMBA DAY UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga (KASHWASA), Joshua Mgeyekwa (kulia), akitoa maelezo jana kwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati (mwenye koti la drafti), alipotembelea jana chanzo cha maji cha Ihelele wilayani Misungwi, mkoani Mwanza wakati wa ziara yake ya kutembelea mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda mkoani Tabora. **PICHA: VICENT TIGANYA**

# Mbivu, mbichi kujulikana wiki hii Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

MACHO na masikio wiki hii yanaelekezwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ambayo itapitia fomu zote za urais na ubunge kwa walioomba kugombea nafasi hizo na kutangaza majina yao.

Tayari vyama vyote 19 vyenye usajili wa kudumu vimeshachukua fomu za kugombea urais, na katika hatua za mwisho za kutembeza fomu katika mikoa 10 kusaka wadhamini 2,000 Bara na Visiwani, ikiwa ni pamoja na kusainiwa na Jaji wa Mahakama Kuu.

NEC ilifungua milango Agosti 5 hadi leo, kwa wagombea urais waliopitishwa na vyama vyao kuchukua fomu za uteuzi kwa nafasi hizo.

Uteuzi wa wagombea hao unatarajiwa kufanyika kesho (Agosti 25), kwa NEC kutangaza majina ya walioteuliwa kwa kiti cha urais, makamu wa rais, ubunge na udiwani. NEC itatangaza nani aliyepitishwa, kukiwa na kicheko au kilio kwa wagombea na vyama vilivyopitisha wanachama wao kupeperusha bendera ya chama chao katika nafasi hizo.

Majina ya wateule yatatangazwa kesho jijini Dodoma katika ofisi za NEC.

Kwa upande wa ubunge, walianza kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa katika ofisi za halmashauri husika Agosti 12, mwaka huu na mwisho ni kesho.

Vyama vya CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo, CUF na NCCR-Mageuzi, vimeshatangaza majina ya wagombea ubunge katika majimbo mbalimbali na uchukuaji fomu unaendelea. Pia wiki hii NEC itatangaza majina ya walioteuliwa na kipenga cha kampeni kitapulizwa Agosti 26 na mwisho itakuwa Oktoba 27, siku ya uchaguzi mkuu itakuwa Jumatano Oktoba 28.

Mchakato wa kupata wagombea hao ulivuta hisia za watu wengi kwa nafasi ya ubunge ndani ya CCM, kutokana na wakongwe, waliokuwa wabunge kwa miaka mingi, walioongoza kwenye kukatwa na waliopata kura chache kupewa nafasi ya kugombea ubunge.

Mwenyekiti wa CCM, Rais John Magufuli, alisema kazi ya kupitia majina 10,367 haikuwa rahisi na kwamba walichambua na kuangalia mambo mengi kabla ya kupitisha kada husika kuwania nafasi hiyo.

Miongoni mwa waliokatwa ni mbunge wa siku nyingi Jimbo la Bariadi na aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Andrew Chenge na aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muheza, Adadi Rajabu. Pia aliyewahi kuwa Waziri wa Nishati na Madini, Willium Ngeleja, aliyewahi kuwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Dk. Charles Tizeba, alikatwa baada ya jina lake kufungana na mwanahabari, Erick Shigongo. Wengine ni aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, aliyefungana na mgombea Charles Kajega.

Waliopitishwa licha ya kuwa na kura chache ni aliyekuwa Mbunge wa Momba, ambaye alihamia CCM Julai, mwaka huu, David Silinde, atakayegombea Jimbo la Tunduma, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Patrabas Katambi, Jimbo la Shinyanga Mjini na Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, atakayegombea Jimbo la Kawe.

Walioachwa uteuzi wa rais na kwenda majimboni na kuangushwa ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, aliyegombea Jimbo la Kigamboni na kushika nafasi ya pili.

Mawaziri wa Serikali ya JPM walioanguka ni wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa. Kwa upande wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), mchakato wa kupata majina ya wagombea ubunge ulikuwa na mvuto baada ya wanawake wengi kusimama katika majimbo mengi, ikiwamo matano ya Dar es Salaam.

Kwa upande wa ACT-Wazalendo, Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, atagombea ubunge katika Jimbo la Kigoma Mjini.


TAARIFA KWA UMMA



DOFRIAN JOHN WALJ

Kampuni ya AKM GLITTERS inapenda kutoa taarifa kwa umma na washirika wake wote kuwa mtajwa hapo juu sio mfanyakazi wa kampuni ya AKM GLITTERS kuanzia tarehe 01 *August 2020.*

Hivyo ndugu Dofrian John Walj sio mwakilishi wa kampuni na hana mamlaka yoyote kufanya biashara au kuwakilisha kampuni ya AKM Glitters.

Kampuni haitohusika na mawasiliano yoyote yatakayo fanywa na muhusika.

*Imetolewa na*
*AKM GLITTERS CO LTD*

AKM GLITTERS COMPANY LIMITED


# JPM aendesha harambee kanisani kuchangia msikiti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli ameendesha harambee ya kuchangia ujenzi wa msikiti wa Chamwino kwenye Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Imakulata, huku akisema huo ndio umoja na upendo wa Watanzania.

Katika harambee hiyo, waumini wa Katoliki na wa madhehebu mengine wamechangia zaidi ya Sh. milioni 48, mifuko ya saruji 48 na malori matano ya mchanga.

Akizungumza jana na waumini wa kanisa hilo, Chamwino Ikulu, Rais Magufuli alisema ujenzi wa kanisa, nyumba ya mapadri na groto katika parokia hiyo umefanywa kwa mafanikio makubwa kutokana na waliojitokeza kuchangia ambao ni waumini wa madhehebu mbalimbali ikiwamo Waislamu.

"Nimefurahishwa sana na umoja wa Watanzania ulioonyeshwa katika ujenzi huu ambao waliojenga na kuchangia fedha wametoka dini mbalimbali, huu ndio umoja kwamba madhehebu yote yanashirikiana kwa umoja na huo ndio upendo," alisema.

Alisema makao makuu ya nchi mahali popote lazima paende na Mungu na kabla ya harambee hiyo alimuomba Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Dodoma, Beatus Kinyaiya, kuruhusu afanye uchangishaji wa ujenzi wa msikiti.

"Kama tulivyoanza kuchangia kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa kanisa hili, nakuomba sana kama utaniruhusu Askofu na kama sitakukwaza tuchange angalau tuanze kujenga msikiti wa ndugu zetu Waislamu," alisema.

Rais Magufuli alisema amefikia hatua hiyo kutokana na umoja ulioonyeshwa na Watanzania na makao makuu kwamba lazima pazungukwe na watu wanaomtukuza Mungu sio wa dhehebu moja bali madhehebu yote.

"Msikiti wao ni mdogo na wapo pale kwa ajili ya kumtukuza Mungu, kuna baadhi ya wasaidizi wangu wengine ni Waislamu, kuna Alhaji humu kwenye wasaidizi wangu ninapoingia humu (kanisani) lazima aingie, lakini inapofika siku yake ya kwenda kumtukuza Mungu nimeambiwa ule msikiti haujawa mkubwa," alisema.

Aliwaomba waumini wa kanisa hilo na wa madhehebu mengine kwa upendo walioonyesha kwenye ujenzi wa kanisa, pia waonyeshe kwenye ujenzi wa msikiti.

"Tutamwomba Paroko aziwasilishe fedha tutakazochangia kwa Shekhe na tukimaliza hivyo tutaangalia na madhehebu mengine kama ni Anglikana, KKKT, Wasabato na mengine ili utukufu wa Chamwino katika kumtukuza Mungu ukasimame katika maisha yote," alisema.

Awali, alisema vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), wameshiriki ujenzi huo na si Wakrito tu bali walikuwa wa madhehebu mbalimbali.

"Nawashukuru wananchi wengine, nilipigiwa na mtu mmoja Dar es Salaam ni Muislamu alitoa Sh. milioni 20, wadau wengi walijitolea, nawashukuru kwa ujenzi huu na usimamizi huu, huu ndio umoja wa Watanzania na upendo," alisema.

Naye Askofu Kinyaiya alisema: "Sikujua kama Rais ana msaidizi wa kila dini na kila kabila, anaonyesha ni mtu wa watu na hana ubaguzi na hili kuchangia msikiti mara ya kwanza nimeona limefanyika kanisani, bila wao kuomba hapa na unatufanya tuendelee kuwa wamoja kama taifa."

Kwa upande wake, Katibu wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Padre Dk. Charles Kitima, alimshukuru Rais kwa uamuzi wa kufanya ujenzi mkubwa wa kanisa ambalo lina historia ya kuwahudumia marais wa Tanzania.zote Afrika, na ukipita kila mahali wanasema tupeni sisi Rais Magufuli aje kwenye nchi yetu," alisema.

"Mlipomuona anaombewa hapa, kila mtu awe mgombea ubunge, udiwani anapita kanisani au msikitini kwake kuombewa, mumuombee na wakija na wengine wanaotaka kwenda Ikulu muwaombee na wengine kwenye vyama vyao muwaombee, tunakuombea Rais nia yako njema ifanikiwe, hiki anachokifanya leo ni kuonyesha namna anavyowapenda Watanzania."

HABARI KITAIFA

## Mpina aanika mafanikio lukuki miaka 5

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa Rais John Magufuli, yamepatikana mafanikio lukuki, kwenye sekta ya mifugo na uvuvi.

Akizungumza jijini Dodoma jana, Waziri Mpina, alisema kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka huu, idadi ya mifugo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Akitolea mfano, Waziri Mpina alisema idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 25.8 hadi milioni 33.4, mbuzi milioni 17.1 hadi milioni 21.29, kondoo milioni 4.8 hadi milioni 5.65, kuku kutoka milioni 37 hadi milioni 83.28.

"Uzalishaji wa maziwa nao umeongezeka kutoka lita bilioni 2.1 mwaka 2015/2016 hadi kufikia lita bilioni 3.0 mwaka 2019/2020, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani 636,559 mwaka 2015/2016 hadi tani 701,679.1 mwaka 2019/2020," alisema Mpina.

Waziri Mpina alisema, katika kipindi hicho serikali ilitunga na kuzifanyia marekebisho sheria na kanuni zilizopitwa na wakati, ambazo zilisababisha usumbufu kwa wananchi.

Alisema sheria na kanuni zilizofanyiwa marekebisho katika sekta ya mifugo ni 27 ikiwamo, kutungwa kwa kanuni mpya ya uogeshaji mifugo pamoja na kutungwa kwa kanuni ya utoaji wa chanjo.

Kwenye uendelezaji wa zao la ngozi, Waziri Mpina alisema serikali imeweka udhibiti wa utoroshaji na udanganyifu katika biashara ya ngozi kwa kutoza asilimia 80 ya usafirishaji wa ngozi ghafi na asilimia 10 ya usafirishaji wa ngozi zilizosindikwa kufikia hatua ya kati.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano serikali imejenga kiwanda kipya cha karanga chenye uwezo wa kuzalisha jozi na soli za viatu 1,200,000 kwa mwaka. Kuchakata ngozi futi za mraba 13,000,000 kwa mwaka pamoja na kuzalisha bidhaa mbalimbali za ngozi.

Kwenye sekta ya uvuvi, Waziri Mpina alisema serikali imefanikiwa kufanya mapitio na kuboresho sheria, kanuni, mipango na tozo mbalimbali zinazosimamia sekta ya uvuvi, ili ziweze kuwa rafiki kwa watumiaji na hivyo kupunguza vitendo vya ukiukwaji wa sheria na kanuni za uvuvi kwa uendelevu wa rasilimali za uvuvi.

Alisema mafanikio mengine ni ujenzi wa bandari ya uvuvi, kuanza kwa uvuvi katika bahari kuu, uzalishaji wa mazao ya uvuvi kwenye maji ya asili, usindikaji na usafirishaji wa minofu ya samaki na mazao mengine ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji, uzalishaji wa samaki katika mabwawa na vizimba.

# Askofu achambua sifa 7 za uongozi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, Beatus Kinyaiya, amechambua sifa saba anazotakiwa kuwa nazo kiongozi anayefaa kuiongoza Tanzania ikiwamo kutokuwa mtoa rushwa na kuweka utaifa mbele.

Askofu Kinyaiya alitaja sifa hizo jana wakati alipokuwa akihubiri Misa Takatifu ya uzinduzi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Imakulata Chamwino, mkoani hapa.

Aliwaomba Watanzania wanapokwenda kupiga kura watazame kiongozi watakayemchagua katika sifa saba alizozichambua kwa kuwa ndoto yao ni kupata viongozi bora na wachapakazi.

Alitaja mambo ya kuangaliwa kwa kiongozi watakayemchagua kuwa ni pamoja na kuwa na roho ya Kimungu.

"Awe mcha Mungu amuogope, kwa kuwa ukiwa mcha Mungu hutafanya ufisadi, dhamira itakusuta, nafsi itakusuta kwa kufanya kitu ambacho hufananii nacho," alisema. Alitaja sifa nyingine ni awe mtu anayeweka Taifa la Tanzania kwanza na akifungua mdomo wake aseme Tanzania kwanza.

"Katika ukorofi wa kutafuta kura ni rahisi sana kutafuta makando kando yatakayomlinda mtu, kama dini vile mtu anasema nipigie mimi kura kwa sababu ni mkristo, au kabila moja, ukiona wa hivyo, hafai yaani taifa moja kwake hamna," alisema.

Aliwataka kutafuta mtu mwajibikaji na awe wa kutenda.

"Kadhalika, awe ni mtu anayetunza tunu za kitanzania na tunu zipo nyingi, amani na mshikamano, akija mtu kutueleza vingine hafai," alisema.

Askofu Kinyaiya alisema kiongozi huyo awe ni mtu ambaye anatafuta uongozi kwa njia halali na kwa kumwaga sera zinazofaa na zinatekelezeka.

"Sipendi kusifia viongozi, lakini awamu ya tano wamewajibika, walisema watafanya mengi wamefanya tunataka watu watakaoendeleza gurudumu kwa njia hiyo," alisema.

Kinyaiya alisema pia awe ni mtu anayejiamini haendi kwa waganga wa kienyeji kupiga bao na kupewa dawa ili ashinde.

"Ukifanya hivyo hufai kwa kuwa unatafuta nguvu ya ziada, utakula takataka na utashindwa," alisema. Pia alisema asiwe mtoa rushwa kwa kuwa kama mtu ana uwezo wa kuongoza atashinda bila kuhonga. "Mbaya zaidi akikupa sahani ya pilau ili umpigie kura thamani yako inakuwa ile sahani ya pilau anakushusha hadi anakufanya sahani ya pilau au chupa ya bia amekuona hivyo, tusinunuliwe kwa vitu vya ovyo bali tutazame sera na uwezo wa mtu," alisema.

Akihamasisha Watanzania kupiga kura, aliwataka waliojiandikisha kupiga kura wahakikishe Oktoba 28, wanajitokeza kwa wingi.

"Wakati mwingine tunachanganya mambo tunachukulia yule mtu ni maarufu atapita tu halafu mnakaa nyumbani, mtu huyo A unayesema maarufu ana watu 20 kwa mfano, na B ana watu watano wanaomkubali wakitoka wote kupiga kura anakuwa na watu watano, na huyu A mwenye watu 20 wakitoka watatu kupiga kura atashinda kweli? Hivyo timiza wajibu wako kapiga kura," alisisitiza. Alimshukuru Rais John Magufuli kwa ujasiri wa kuchangisha upanuzi wa kanisa hilo kwa kuwa waumini wa kanisa hilo waliweka mipango kwa kuchanga, lakini hawakufanikiwa kuanza ujenzi wake.



Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Richard Kayombo (kulia), akiongea baada ya kufunga semina ya wadau kuhusu mfumo mpya wa uwakilishaji ritani za kodi kwa njia ya kielektroniki jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TABOA yalia ukatishaji tiketi kimtandao

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), kimesema kuna umuhimu kwa serikali kupitia upya na kushirikisha wadau kikamilifu kuhusu kanuni za sheria ya usafiri, ili kuondoa tozo zitakazoongeza gharama za uendeshaji kwa usafirishaji wa abiria.

Kwa mfumo mpya, kwa sasa tiketi za usafiri zitakatwa kielektroniki kwa abiria wote, jambo ambalo litaondoa usumbufu na udanganyifu kwa wasafiri.

TABOA ilitoa malalamiko hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao baina yake na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC).

Kaimu Katibu Mkuu wa TABOA, Joseph John, alisema ni vyema mamlaka hizo zikafuatilia kwa kina na kufafanua tozo ya asilimia mbili ya gharama za uendeshaji wa mfumo ulioletwa kwao na LATRA.

Alisema TABOA iliwasilisha kwa wazabuni waliokuwa tayari kufanya kazi hiyo kwa tozo ya asilimia 0.7 ya gharama ya tiketi, lakini hawakukubalika na sasa kumejitokeza mzigo wa uendeshaji.

Jingine ni malipo kupitia T-Pesa ambapo mmliki wa basi atalazimika kuweka kiasi cha fedha kwenye mashine ya kukatia tiketi (POS), ili amkatie abiria tiketi. Kwa mujibu wa John, ni vyema mamlaka zikafafanua jinsi zilivyojipanga kufanya uwiano wa kisheria katika kuendesha mfumo huo ili isifike wakati wasafirishaji wakatozwa faini mara mbili kwa kosa moja.

"Kwa taswira ya haraka tunazo mamlaka mbili na kila moja ina majukumu tofauti ya kisheria. TRA itamtaka mmiliki kuhakikisha anatoa risiti halikadhalika LATRA inamtaka mmiliki kutoa tiketi, hivyo tutakuwa na risiti na tiketi, ni vema tuwe na hoja zenye nguvu ili kuzishauri mamlaka kuzingatia haya," alisema John.

Jambo jingine lililolalamikiwa na TABOA ni tozo ya asilimia 0.5 ya mauzo ya tiketi inayotozwa na LATRA kupitia mfumo huo, na kwamba wanaona si sahihi kwa kuwa mamlaka hiyo haitoi huduma yoyote kwao na jukumu lake la msingi ni udhibiti.

Aidha, TABOA ililalamika kutoshirikishwa kwenye mchakato wa kupata mzabuni atakayeendesha mfumo wa ukatishaji tiketi pamoja na kuzuia leseni za mabasi kama hawatajiunga na mfumo huo, na kwamba ni vyema kukawa na maelewano ya wadau. Baada ya majadiliano ya muda mrefu, wasafirishaji hao walilazimika kwa kauli moja kutomtambua mzabuni wa mfumo aliyetafutwa na LATRA bila ushiriki kikamilifu wa wadau.

Pia waliazimia mashine za kutolea risiti za EFD ziruhusiwe kutumika kukatishia tiketi ukiwa mwafaka wa jambo hilo hautapatikana na kuitaka LATRA kujitoa kwenye uendeshaji wa mfumo wa ukatishaji tiketi hizo na kazi hiyo iwe chini ya TRA.

Walitaka kusogezwa mbele muda wa kuanza kutumia mfumo mpya wa kielektroniki, ili kutoa nafasi ya kuelimisha watumiaji na wananchi kwa ujumla.

Akijibu hoja hizo, Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Barabara wa LATRA, Johansen Kahatano, alikubaliana na baadhi ya hoja za wadau hao ikiwamo kuongeza muda ili kuruhusu kutolewa kwa elimu zaidi.

"Tutatafuta nafasi kukutana na uongozi wenu ili tuone jinsi gani tunaweza kulifanya hili, tunawahakikishia kila mmoja tutamfikia. Kuhusu suala la kuzuia leseni kwa wasiojiunga na mfumo huu pia litasogezwe mbele," alisisitiza Kahatano.

Kuhusu tozo ya asilimia 0.5, alisema ni takwa la kisheria lililowekwa na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini ya mwaka 2019, ambalo ni lazima litekelezwe.

## Uholanzi yakana Rabo kuondoa hisa NMB

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Uholanzi imeihakikishia Tanzania kuwa benki ya Rabo ya nchi hiyo, haina mpango wa kuondoa hisa zake ndani ya benki ya NMB kama ilivyoripotiwa katika baadhi ya mitandao ya kijamii.

Ofisa wa Ubalozi wa Uholanzi nchini (anayeshughulikia mambo ya uchumi), Mathij van Eeuwen, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma wakati akipokea gawio la Sh. bilioni 16.8 kutoka NMB.

Tukio hilo lilimhusisha Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, Msajili wa Hazina, Athuman Mbutuka, Mwenyekiti wa Bodi ya NMB, Dk. Edwin Mhede na Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna pamoja na watumishi wa Wizara ya Fedha.

Mathij alieleza kinachoendelea ni kuzingiza hisa zake katika mtandao wa Arise ambao unamilikiwa na benki ya Rabo ya Uholanzi, lakini si kuzitoa hisa hizo kama taarifa zilivyosambazwa.

Alimweleza Waziri Mpango kuwa bado wana imani kubwa na NMB, hivyo hawajafikiria kuondoa hisa zao na kuwa mawazo hayo hayapo kwa sasa ndani ya benki ya Rabo.

Alisema kinachoendelea ni utaratibu wa kawaida wa kuweka hisa hizo ndani ya mtandao wao, jambo alilosema ni la kawaida kufanyika, lakini lisihusishwe na kujitoa wakati huu ambao bado wana imani na NMB na wanatengeneza faida.

"Hayo maneno kuwa tunataka kujitoa siyo ya kweli, sisi hatuwezi kujitoa, tuliitaarifu serikali kuhusu kuzihamisha hisa na kuzikabidhi katika mtandao wa Arise, ambao upo ndani ya benki ya Rabo, hivyo ndivyo tujuavyo na si vinginevyo," alisema Mathij.

Akizungumzia utendaji wa benki ya NMB chini ya Ofisa Mtendaji mkuu, Ruth Zaipuna, alisema hawana hofu na mtendaji huyo mkuu huyo kuwa katika kipindi alichokaimu nafasi hiyo benki ilifanya vizuri, hivyo hawaoni kama kuna shida katika usimamizi na utendaji wake.

Dk. Philip Mpango alipongeza uamuzi wa benki ya Rabo wa kuendelea kuiamini Tanzania katika benki ambayo nao wana hisa nyingi na hasa kitendo cha kukubaliana na uamuzi wa kuwa na mtendaji mkuu Mtanzania kwa mara ya kwanza.

Alisema Serikali ya Tanzania itaendelea kuheshimu na kutengeneza mazingira rafiki kwa wawekezaji ikiwamo katika sekta ya fedha kwa kuwa inaamini katika njia hiyo kuliko kuendelea kuwa ombaomba kwa kipindi cha karibu miaka 60 baada ya Uhuru. Waziri alisema kwa sasa wanataka ubia na uwekezaji kwa kuwa unaingizia serikali fedha nyingi ambazo zinakwenda kwenye miradi mbalimbali akitole mfano wa Sh15. 2 bilioni ilizopata serikali kama gawio la asilimia 31.8 ya hisa inazomiliki ndani ya benki hiyo.

Kuhusu kuhamisha hisa hizo kwenda katika mtandao mwingine, waziri alisema wako katika hatua za kukamilisha taratibu za kufanya hivyo kama walivyokubaliana na wabia wao hao ili kukidhi mahitaji yanayotakiwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema mbali na Sh. bilioni 15.2 ilizopata serikali na Sh. bilioni 16.8 za Rabo benki ya Uholanzi, wawekezaji wengine ambao ni taasisi na watu binafsi kwa pamoja walipata gawio la Sh. bilioni 13.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania – TIC, Dk. Maduhu Isaac Kazi (kulia), akijadiliana jambo na mwakilishi wa kampuni ya Elsewedy ya Misri, Injinia Ibrahim Qamar, juzi katika ofisi za TIC jijini Dar Es Salaam. katikati ni Mkuu wa Idara ya Uwezeshaji kwa Wawekezaji, Revocatus Arbogast Rasheli. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Lissu apata wadhamini zaidi ya 10,000

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA urais wa CHADEMA, Tundu Lissu, amesema katika safari ya kusaka wadhamini katika mikoa 10 ya Bara na Visiwani, amepata wadhamini zaidi ya 10,000.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam jana, alisema sheria ya uchaguzi inataka mgombea kuwa na wadhamini wasiopungua 2,000, na kwamba hakuna zuio la mgombea kupata wadhamini zaidi.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi wanatakiwa kupata wadhamini milioni 10, na inakataza kupeleka chini ya 2,000 na wanaweza kuwa zaidi kwa kadri mgombea alivyodhaminiwa.

Kwa mujibu wa Lissu, kilichofanywa na chama hicho kwa siku 12 na mgombea urais kusaka kura za maoni, si kampeni, na kwamba hakuna sheria inayozuia kwa kuwa muda wa kampeni bado haujaanza. Aidha, alisema ana kesi sita katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, na zilifunguliwa mwaka 2016/17, na zilikuwa zimesimama na alivyorejea nchini, zilianza na kupangiwa kusikilizwa Agosti 26, mwaka huu, ambayo ndiyo siku ya kujua matokeo ya walioteliwa kugombea urais.

Aidha, Lissu alieleza kusikitishwa na matukio ya kuungua kwa ofisi za CHADEMA mkoani Mbeya na Arusha, pamoja na vurugu kwa msafara wake kuvamiwa akiwa Jimbo la Hai, mkoani Kilimanjaro.

Alisema mgombea ubunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, John Mwenegoha, alinyimwa fomu za uteuzi kwa sababu zisizoeleweka, huku wasiowateule wa chama kupewa fomu za kugombea katika majimbo ya Kigamboni, Kibamba, Mbagala na Kilombero, na baada ya ufuatiliaji fomu zilipatikana.

"Tunaitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuchukua hatua kwa matukio ya wagombea wa upinzani kunyimwa fomu, na wasimamizi wa uchaguzi wanaofanya hivyo kufukuzwa kazi kwa kuwa wameshaonyesha upande," alisema.

Matukio mengine ni mgombea wa Jimbo la Mwihambe, Filex Mkosamali na Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi, kukamatwa kwa madai alikuwa na maandamano na baadaye waliachiwa.

## CCM, CUF, ACT wachangamkia fomu za ubunge

**Na Waandishi Wetu**

WAGOMBEA ubunge kwa tiketi za CCM, ACT-Wazalendo na CUF jana waliendelea kuchukua fomu kutoka kwa wasimamizi wa uchaguzi katika halmashauri mbalimbali nchini.

Wagombea hao wakiwa wameambatana na wanachama wao walichukua fomu kwa nyakati tofauti na kuahidi kufanya kampeni za amani bila kuvunja kanuni, taratibu na sheria za uchaguzi.

Majimbo ya Singida Mashariki na Magharibi, Miraji Mtaturu wa Jimbo la Singida Magharibi, Elibariki Kingu walichukua fomu za kuwania ubunge kwa mara nyingine kwa tiketi ya CCM.

Msimamizi wa Uchaguzi Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Justice Kijazi, alisema jumla ya wagombea 13 walichukua fomu na aliwataka kufanya kampeni za kistaarabu.

"Kwa niaba ya Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) sisi tupo na tunawakaribisha na yapo masharti mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi huu moja ya mambo ambayo mtapewa ni kanuni za maelekezo lakini tunaomba uchaguzi wetu uwe huru na haki ambao hauna vurugu kama vile tunavyosema," alisema Kijazi.

Jimbo la Kongwa; Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliyechukua fomu katika Jimbo la Kongwa, na kuahidi kuzingatia masharti na kutafuta wadhamini. Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Kongwa, Dk. Omary Mkulo, alisema tangu kuanza utoaji fomu Agosti 12 mwaka huu wagombea wanne walichukua fomu.

Aliwataja wagombea wengine kuwa ni Emanuel Ng'ombilo wa SAU, Bwabwio Mbahuka wa ADC na Edyson Mbennah wa CHADEMA.

Jimbo la Chemba, mgombea ubunge wa CCM, Mohamed Moni, alichukua fomu na kuahidi kuweka mikakati ya kuboresha elimu na afya.

Jimbo la Chalinze, mgombea ubunge Jimbo la Chalinze kwa tiketi ya CCM, Ridhiwani Kikwete, alichukua fomu kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Ramadhani Possi, kuwania nafasi hiyo.

Wakati akichukua fomu hiyo, alisema ipo miradi mikubwa ambayo inatakiwa kusimamiwa katika jimbo hilo itakayoinua uchumi kwa Halmashauri ya Chalinze na Mkoa.

Jimbo la Kisarawe, mgombea wa chama hicho Jimbo la Kisarawe, Selemani Jafo, alishukuru Halmashauri Kuu ya chama hicho kwa kumwamini na kumpa ridhaa ya kupeperusha bendera katika jimbo hilo. Jimbo la Lindi Mjini, Isihaka Mchijta, alichukua fomu kwa tiketi cha Chama cha ACT-Wazalendo katika Jimbo la Lindi Mjini, huku msimamizi wa uchaguzi Manispaa ya Lindi, Baprista Kihanzi, akiwataka kufuata sheria na kanuni zilizopo na kampeni za kistaarabu.

Pia, Salum Bar'wani alichukua fomu kwa tiketi ya CUF. Msimamizi huyo aliwataka wanasiasa kuhakikisha wanapokuwa kuendesha siasa za kiustaarabu kwa kunadi sera zao.

Jimbo la Mchinga, Hamidu Bobari anagombea kwa tiketi ya CUF na wote walimthibitishia msimamizi wa uchaguzi kuwa watafanya kampeni za kiustaarabu.

■ **Imeandikwa na Said Hamdani (LINDI), Dotto Mwaibale (IKUNGI), Na Julieth Mkireri, (CHALINZE), Ibrahim Joseph, KONGWA, Renatha Msungu (CHEMBA)**

# Silinde afichua usaliti CCM ulivyompatia ushindi 2010

**Na Thobias Mwanakatwe**

ALIYEKUWA Mbunge wa CHADEMA katika Jimbo la Momba, David Silinde ambaye sasa ni mgombea mteule wa CCM Jimbo la Tunduma Mjini, amefichua siri kwamba ushindi wake wa mwaka 2010 ulitokana na kupewa magari na fedha kutoka kwa baadhi ya wanaCCM waliokuwa wakikisaliti chama hicho.

Alisema hayo juzi katika mkutano wa wanaCCM uliofanyika Mjini Tunduma, uliokuwa na lengo la kuwatambulisha wagombea ubunge katika majimbo ya Momba na Tunduma sambamba na kuvunja makundi na kuhimiza mshikamano ili chama kiweze kuibuka na ushindi katika Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

"Mimi ushindi wangu mwaka 2010 nikitoka shuleni mwanafunzi na wakati huo CCM walikuwa wamepita kata nane bila kupingwa, wagombea wa CCM walioshindwa ndio walinipa gari na fedha zikanisaidia kwenye kampeni," alisema.

Hata hivyo, Silinde alisema hawezi kuwataja majina wana CCM waliompa fedha na magari kwa sababu hautakuwa ubinadamu.

"Siwezi kuwataja mlionipa pesa na magari, ni siri yangu kwa sababu nikiwataja nitakuwa nimekosa ubinadamu, lakini mlinipa ushindi kwani CHADEMA walikuwa na wanachama wangapi, wakati tunakwenda kushinda 2010 CCM ilikuwa na mitaa 122 na CHADEMA 6 tu na vitongoji vyote vilikuwa CCM, hivyo mtu anashindaje uchaguzi, ambayo ni kama miujiza, ninyi ndio mnatoa ushindi," alisema Silinde.

Alisema hivi sasa wanaCCM na wananchi wa Tunduma kwa ujumla watembee kifua mbele kwani CCM inakwenda kushinda ubunge, udiwani na kata zote na ile furaha ya CCM iliyokuwapo miaka yote itarudi mara mbili yake.

Aliongeza kuwa ili CCM iweze kushinda katika uchaguzi wa mwaka huu, kinachohitajika ni umoja na mshikamano.

"Hivi sasa kama kuna kitu wenzetu wanaomba ni mpasuko ndani ya CCM, ukipasuka hapa CCM inakwenda kuwa benchi miaka 15, maana yake miaka 10 ya mwanzo na kuongeza mitano," alisema Silinde.

Alisema anawaachia wanaCCM uchaguzi huo.

Silinde aliwaomba wanaCCM watambue kuwa yeye ni mwenzao na sio adui, na wala hakuja CCM kutaka kukiharibu chama, bali nia yake ni kukitengeneza.

"CCM ni chama kikubwa kina mambo mengi na ndio maana Rais wakati akitangaza matokeo alisema wale watakaopingana na uteuzi wakaangalie kwanini hawakuteuliwa," alisema.

# JUKATA kuja na sera kushinikiza uteuzi sawa

**Na Mwandishi Wetu**

JUKWAA la Katiba Nchini (JUKATA), limeonyesha wasiwasi wake kwa vyama vya siasa katika uteuzi wa safu za viongozi nafasi ya watoa maamuzi kutozingatia usawa wa kundi maalumu.

Jukwaa hilo limesema hali kwenye vyama hivyo inatisha na linashangaa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutovikumbusha vyama hivyo kuzingatia usawa wa uteuzi kwa kundi maalumu la vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Kutokana na upungufu huo, Mjumbe wa Bodi ya JUKATA, Deus Kibamba, alisema jukwaa hilo lipo katika maandalizi ya rasimu ya sera ya kitaifa ya ushirikishwaji vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwenye uteuzi ili sauti za wanyonge ziweze kusikika.

Akiongea na wahariri na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Kibamba alisema katika utafiti wao wamebaini kuwa kundi hilo kutopewa haki sawa licha ya baadhi ya taasisi kuwa na sera hiyo ikiwamo Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), inayojulikana kama 'Social inclusion policy' (Sera jumuishi ya kijamii).

Alisema nia ya kuwa na sera hiyo ni kutaka kundi maalumu lililotajwa linapata haki sawa katika uteuzi tofauti na inavyofanyika sasa.

Alisema hata kwenye nafasi 10 za uteuzi za urais, mmoja anapopoteza sifa mbadala wake uwe kundi lile lile kwa mfano anapofariki, tofauti na sasa anateuliwa mtu asiye wa kundi hilo.

Kuhusu uteuzi wa wagombea katika vyama vya siasa, Kibamba alisema kundi maalumu na asilimia 30 haikuzingatiwa kama inavyoeleza Katiba ya nchi.

"Kwanini inapotokea ubaguzi wa aina hiyo kwenye vyama, NEC na ZEC isirudishe majina kwenye vyama hivyo kama Ibara ya 13 ya Katiba inavyosema hakuna ubaguzi kwenye uteuzi (upande wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu)," alisema.

Akizungumzia kundi la viti maalumu, Kibamba alisema, lengo lake lilikuwa ni kuwapa uzoefu wanawake ili baadaye waende kugombea kwenye majimbo, lakini kwa ilivyo sasa havina utaratibu maalumu wa wazi. "Viti maalumu ni kama unakwenda field (mafunzo kwa vitendo), lakini kuna watu wapo zaidi ya miaka kumi hawataki kwenda kwenye majimbo na kupoteza lengo lake la kundi lingine kuingia na kujifunza," alisema.

Akifafanua mapendekezo ya rasimu ya sera hiyo, alisema vyama vya siasa vina wajibu wa kuteua vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika majimbo, pia fedha za kuwezesha wagombea wa kundi hilo majimboni.

Vyama pia vina wajibu wa kuweka mbadala wa kundi hilo na Ofisi ya Msajili kuandaa utaratibu wa kulazimisha vyama vya siasa vinavyokwenda kinyume kwa mujibu wa Katiba. Kadhalika, alisema katika mapendekezo hayo NEC na ZEC ziandae fomu kulazimisha uteuzi kwenye vyama vya siasa uwe asilimia 30 kwa wanawake na pia NEC ianzishe sera ya taifa ya ushiriki wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema rasimu ya sera hiyo inatarajiwa kuwasilishwa baada ya kukamilika kwa ushirikishwaji wa wadau wote.



Sehemu ya watu waliojitokeza katika zoezi la uchangiaji damu lililoendeshwa na Jumuiya ya Khoja Shia Ithnasheri kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Damu Salama na Hospitali ya Ebrahim Haji jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mrema: Mbatia, Kimei hawataniweza Vunjo

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA ubunge katika Jimbo la Vunjo, Augustino Mrema, amesema hatishwi na wagombea wenzake James Mbatia (NCCR-Mageuzi) na Dk. Charles Kimei wa CCM waonekane kuwa ndio tishio katika jimbo hilo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza katika mahojiano maalum na gazeti hili jana, Mrema alisema ameshangazwa kuona katika vyombo vya habari kwamba wagombea ambao ni tishio katika Jimbo la Vunjo ni Mbatia na Dk. Kimei.

Alisema jimbo hilo lina wagombea watano waliochukua fomu kutoka vyama mbalimbali, na kwamba watu kudai kuwa Mbatia na Dk. Kimei ndio tishio, hizo ni propaganda zisizo na mashiko ambazo hazijafanyiwa utafiti kwenye kana wagombea hao wawili tu ndio tishio. Mrema ambaye alishawahi kuwa mbunge katika jimbo hilo, alisema wananchi wa Vunjo safari hii hawadanganyiki wanamtaka yeye (Mrema) kutokana na kuwa na rekodi nzuri ya kuwaletea maendeleo.

"Sitishwi na propaganda ambazo hazijafanyiwa utafiti, wananchi wananitaka mimi kwa sababu nina rekodi nzuri, wasijaribu kuwanyeshwa sumu wananchi wakati wanafahamu sumu haionjwi," alisema Mrema ambaye aligombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara tatu mwaka 1995, 2000 na 2005.

Mrema ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Tanzania Labour (TLP), alisema chama chake hakijaweka mgombea urais kwenye uchaguzi huu kwa sababu mgombea urais wa CCM, Rais John Magufuli anatosha. "Rais Magufuli amefanya mambo mazito ya maendeleo kwenye nchi hii, chama changu kitamsaidia kampeni ili achaguliwe tena aendelee kuwa rais," alisema. Mrema alisema wananchi wa Vunjo ambao ni wapenda maendeleo, wanatambua kuwa mbunge pekee atakayeweza kufanya kazi vizuri na Rais Magufuli ni yeye (Mrema), hivyo hawawezi kumuacha katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mikataba wachezaji wa mkopo haya yazingatiwe TFF, klabu

**KLABU** za Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili Tanzania Bara bado zipo katika harakati za kuimarisha vikosi vyao, baada ya dirisha la usajili kufunguliwa tangu Agosti Mosi, mwaka huu, huku likitarajiwa kufungwa rasmi mwishoni mwa mwezi huu.

Aidha, wigo wa usajili umeongezeka zaidi baada ya Alhamisi iliyopita dirisha la usajili Zanzibar kufunguliwa huku likitarajiwa kufungwa Septemba 19, mwaka huu, hivyo milango kuwa mingi zaidi kwa klabu za Bara na visiwani kuweza kujiimarisha kabla ya msimu mpya wa 2020/21 kwa Tanzania Bara kuanza hapo Septemba 6, mwaka huu.

Tunafahamu katika kipindi hiki, wapo baadhi ya wachezaji watatolewa kwa mkopo ili kwenda kupata nafasi ya kucheza zaidi, hivyo umakini unahitajika zaidi kwa kufuatwa taratibu zote ili kuepuka mvutano kama uliotokea katika dirisha dogo la usajili.

Tumelazimika kukumbusha hilo hasa tukikumbuka kilichotokea kati ya Azam FC na Klabu ya Polisi Tanzania kuhusu mkataba wa mshambuliaji Ditram Nchimbi, aliyekuwa akitakiwa kusajiliwa na Yanga baada ya klabu yake mama, Azam kuridhia.

Kama ilivyokuwa kwa klabu hizo mbili, Nchimbi alikuwa akichezea Polisi Tanzania kwa mkataba wa mkopo akitokea Azam FC, ambao awali ulielezwa kwamba ulikuwa wa msimu mzima.

Lakini kwa mujibu wa Polisi Tanzania, makubaliano yao na Azam yalikuwa kumtumia mchezaji huyo hadi mwishoni mwa msimu huu uliomalizika ndipo arejee klabuni kwake, na hapakuwa na kipengele chochote kinachoiruhusu Azam kumchukua katikati ya msimu, jambo ambalo liliwafanya kupaza sauti za kumzuia kuuzwa Yanga kabla ya baadaye kuketi na kuyamaliza kiutu uzima. Kwa upande wa Azam FC ilieleza kwamba hapakuwa na kipengele chochote kinachoeleza kwamba hawataruhusiwa kumchukua mchezaji wao watakapomhitaji, huku wakiamini ni sawa na mtu kumpa mtoto wako amlelee, jambo ambalo unapomhitaji unaweza kumchukua wakati wowote.

Hata hivyo, Azam ilieleza baada ya Yanga kufika dau la kumnunua Nchimbi, ilitoa kipaumbele kwa Polisi Tanzania kama inamhitaji jumla imnunue, lakini ikawaeleza haina uwezo huo na kuwaruhusu kuendelea na taratibu zingine za kumuuza.


Hapo ndipo tunapoona kuna haja ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), katika dirisha hili kubwa la usajili kuwa makini katika suala zima la mikataba ya wachezaji hususan hawa wa mkopo ili baadaye kutokuleta utata pindi klabu mama itakapomhitaji mchezaji wake iwe katikati ya msimu ama mwishoni.

Utata uliojitokeza katika mkataba huo wa mkopo wa Nchimbi ni wazi makubaliano mengi yalikuwa ya mdomo tu na si kwa maandishi, hivyo unabidi uwe fundisho kwa klabu zote zinaponunua wachezaji kwa mkopo, lakini TFF inapaswa kuhakikisha vipengele vyote muhimu vinazingatiwa kabla ya kuipokea.

Nipashe tunatambua mikataba ya mikopo kwa wachezaji huwa ina vipengele vingi muhimu na huwa hawatolewi kiholela kama ambavyo klabu zetu nchini zinafanya, kwani; awali kabisa ni lazima mkopo huo uainishe wazi ni wa muda gani na nani atamlipa mshahara mchezaji husika. Kingine cha kuzingatiwa mkataba wa mkopo unaweza kuwa na kipengele kwa klabu mama kumhitaji mchezaji wao muda wowote ama hataruhusiwa kucheza dhidi ya klabu yake hiyo pindi timu hizo zitakapokutana, lakini pindi itakapotaka kumuuza, klabu anayoichezea kwa mkopo ipewe nafasi ya kwanza kumnunua na ikishindwa ama kutohitaji tena huduma yake ndipo auzwe kwingineko.

Lakini, katika mikataba hiyo ya mkopo ni lazima iainishe endapo klabu mama inaweza kumchukua wakati wowote inapomhitaji ama kuonyesha ni lini hasa utakuwa ukomo wa mkataba huo wa mkopo. Hayo ni machache tu katika mengi yanayopaswa kuwekwa wazi katika mikataba ya wachezaji wanaotolewa kwa mkopo, Hivyo wakati huu usajili ukiendelea, TFF na klabu kuna haja ya kukaa chini na kufuata taratibu hizo kwa kuhakikisha vipengele hivyo muhimu vinakuwapo katika mikataba ili kuepusha mivutano kama iyotokea kati ya Polisi Tanzania na Azam FC wakati ikitaka kumuuza Nchimbi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kushirikiana choo wanaume, wanawake doa Simba Day

Na Adam Fungamwango

**ILIKUWA** ni siku ya kukumbukwa kwa wanachana, mashabiki wa Simba na Tanzania nzima, walipoungana kusherehekea tamasha lao la kila mwaka kufanya shughuli za kijamii, pamoja na kutambulisha kikosi kipya cha msimu husika.

Ilikuwa ni Jumamosi nzuri, wanachama na mashabiki wa Simba walipokusanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam ambao walibahatika kuhudhuria, lakini kuna waliokuwa wakifuatilia matangazo redioni na kwenye runinga pia.

Naipongeza klabu ya Simba na wasimamizi wa Uwanja wa Mkapa kwa kuandaa tamasha hilo kuwa la kuvutia mno. Inawezekana kabisa tangu Simba ianze kuandaa matamasha hayo kila mwaka na kuyaita 'Simba Day', la mwaka huu lilifana zaidi.

Hata hivyo, pamoja na mambo mengi kuwa mazuri, lakini kulikuwa na kasoro kadhaa ambazo hazipashwi kutozungumzwa, lakini sina budi kuzizungumza ili tuendapo zifanyiwe kazi. Nia ni kujenga na kuondoa mapungufu yasiyo ya lazima yanayojitokeza na si kubomoa.

Kwanza kabisa ni upande wa Simba ambao ulijikosesha mapato mengi kutokana na urasimu mkubwa kwenye upatikanaji wa tiketi.

Watu walitoka kwenye mikoa mbalimbali wakidhani watapata tiketi kwa urahisi, lakini badala ya kununua tiketi kwa utaratibu ambao wanaoutambua, wakakutana na utaratibu tofauti na waliouzoea kama vile kuwa na kitambulisho cha Taifa au namba za NIDA ili kupata tiketi.

Si mbaya kufanya hivyo, lakini utaratibu huo ulikuwa ni wa ghafla sana na watu waliujua pale tu walipofika vituoni. Hawakuambiwa kabla. Lakini hii ilisababisha mtu mmoja kukaa muda mrefu kabla ya kupata tiketi. Hali ilipozidi kuwa mbaya na msongamano kwenye vituo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara aliamua kuongea na wanachama na mashabiki kupitia akaunti yake ya mtandao wa kijamii kuwaambia kuwa wameamua kubadilisha staili ya uuzaji wa tiketi na sasa mtu atanunua moja kwa moja bila kupitia utaratibu wa awali.

Kama nilivyosema awali, utaratibu wa mwanzo inawezekana ulikuwa mzuri tu, lakini ilitakiwa kwanza watu wote waeleweshwe kabla, lakini haikutakiwa ifanyike kwenye tamasha kama hilo ambalo huvutia watu wengi. Majaribio yangeanza kwenye mechi za kawaida tu ambazo haziingizi mashabiki wengi.

Athari ya hilo, tuliona upande wa kusini kulikuwa na mapengo, ambayo nadhani yasingekuwapo kama kusingekuwa na kile kilichojitokeza kwenye ukataji wa tiketi. Kingine cha kushirikiana ni wanaume na wanawake kutumia choo kimoja. Upande wa Kaskazini Magharibi mwa uwanja kulikuwa na sehemu ambayo wanaume na wanawake walikuwa wanatumia choo kimoja.

Na choo ambacho walikuwa wanatumia ni cha wanawake. Choo cha wanaume kilikuwa kimefungwa, haijulikani kama kilikuwa na matatizo gani. Na kama kilikuwa kibovu kwa nini hakijatengenezwa kwa ajili ya maandalizi ya tamasha hilo? Hali hii haikuwa nzuri sana kwa wanawake ambao walishangaa kuona wakiwa pamoja na wanaume. Mara zote, mazingira ya vyoo vya wanawake ni tofauti na vya kiume, hivyo ikaleta usumbufu mkubwa kwa kinamama na watoto wao waliokuwa wamekusanyika kwa wingi uwanjani.

Hali hii imetia doa kubwa kwenye mchezo wa soka ambao kwa sasa umepiga hatua kubwa kwa kupendwa na wanawake wengi tofauti na zamani. Kwa sasa kinamama wengi wamekuwa wakijumuika uwanjani kuzishangilia timu wanazozipenda, hivyo ni wajibu wa wasimamizi kuwalinda, ikiwa ni pamoja na kuwapa huduma zao muhimu kama watoto wa kike.

Kitendo cha kuchanganyika na wanaume kinaweza kuwakatisha tamaa na kuwaogopesha kuja viwanjani kwa kuhofia hilo. Tukumbuke kuwa wanawake wameumbwa na aibu, lakini kibinadamu pia si vizuri. Shirikisho la Soka nchini (TFF), linabidi liangalie sana suala hili, kwani mara kwa mara limekuwa likisisitiza mashabiki kwenda viwanjani, lakini moja ya mambo ambayo ya kuhamasisha ni lazima kuwe na mazingira mazuri hasa kwa mashabiki wapya wanaoanza kuvutiwa kwenda viwanjani hususan wanawake kwa kuwawekea mazingira rafiki ikiwa ni pamoja na miondombinu hiyo ya choo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO KATIKA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (5) YA UONGOZI WA RAIS MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI ILIYOTOLEWA NA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI, MHE. LUHAGA JOELSON MPINA

**TAREHE 23 AGOSTI, 2020 DODOMA**

**AGOSTI, 2020**
**DODOM**

# MAFANIKIO SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

**1.0 UTANGULIZI**

Sekta ya Mifugo ina fursa kubwa katika kuchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kiuchumi kwa jamii na kuongeza kipato kwa Watanzania hususan wanaotegemea mifugo. Aidha, Wizara imeweka mazingira mazuri yanayotoa fursa za kuongeza kipato na ajira kwa wafugaji wakubwa na wadogo kufuga kibiashara na kuongeza ajira. Sekta ya Mifugo ilichangia **asilimia 7.4** ya Pato la Taifa na imekua kwa **asilimia 5** kwa Mwaka 2019.

Vilevile, Sekta ya Uvuvi ni moja kati ya sekta muhimu za kiuchumi hapa nchini. Shughuli za uvuvi hapa nchini zinahusisha uvuvi kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe maji. Katika mwaka 2019, Sekta ya Uvuvi ilichangia **asilimia 1.71** ya Pato la Taifa na imekua kwa **asilimia 9.2**. Aidha, Sekta ya Uvuvi huchangia katika kuwapatia wananchi uhakika wa chakula, lishe, kuongeza kipato, fedha za kigeni na kupunguza umaskini.

**2.0 HALI HALISI YA SEKTA YA MIFUGO**

**2.1 Mwenendo wa Idadi ya Mifugo**

Idadi ya mifugo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kati ya mwaka 2015/2016 na 2019/2020 kama ifuatavyo:-

(a) Ng'ombe kutoka **milioni 25.8** hadi **milioni 33.4**
(b) Mbuzi kutoka **milioni 17.1** hadi **milioni 21.29**
(c) Kondoo kutoka **milioni 4.8** hadi **milioni 5.65**
(d) Kuku kutoka **milioni 37.0** hadi **milioni 83.28**

**2.2 Mchango wa Sekta ya Mifugo Katika Uchumi**

(i) Mchango wa Sekta ya Mifugo umeongezeka kutoka **Shilingi 7,158,457,000,000** mwaka 2015/2016 hadi **Shilingi 10,344,727,000,000** katika mwaka 2019/2020.
(ii) Mapato ya Serikali yameongezeka kutoka **Shilingi bilioni 12.6** mwaka 2015/2016 hadi **Shilingi bilioni 44.9** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 256.**

**2.3 Uzalishaji na Biashara ya Mazao ya Mifugo**

(i) Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka **lita bilioni 2.1** mwaka 2015/2016 hadi kufikia **lita bilioni 3.0** mwaka 2019/2020;
(ii) Uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka **tani 636,559** mwaka 2015/2016 hadi **tani 701,679.1** mwaka 2019/2020; na
(iii) Uzalishaji wa ngozi umeongezeka kutoka **Kilo 15,389,129** mwaka 2015/2016 kufikia **Kilo 18,242,835** mwaka 2019/2020.

**3.0 MABORESHO YA SHERIA NA KANUNI KATIKA SEKTA YA MIFUGO**

**3.1 Maboresho ya Sheria**

Serikali imeamua kutunga na kuzifanyia marekebisho **Sheria na Kanuni** zilizopitwa na wakati ambazo zilisababisha usumbufu mkubwa na malalamiko kutoka kwa wananchi. Marekebisho hayo yameboresha mazingira ya uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake na kuongeza mchango katika Pato la Taifa, ajira, na ukuaji wa uchumi nchini. Jumla ya Sheria na Kanuni zilizofanyiwa Marekebisho katika Sekta ya Mifugo ni **27.** Baadhi ya Sheria na Kanuni hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Kutungwa kwa Kanuni mpya ya Uogeshaji mifugo **(Acaricide Application and Management)** 2019, GN No.955. Kanuni hii imeweka mwongozo na usimamizi thabiti wa uogeshaji mifugo nchini na kuweka bei elekezi ya kuogesha mifugo ambapo ng'ombe mmoja kwa mchovyo ataogeshwa kwa shilingi 50 tu badala ya shilingi 500 zilizokuwa zikitozwa kabla ya Kanuni hii; Mbuzi na Kondoo ni shilingi 10 kwa mchovyo badala ya **shilingi 100** ilivyokuwa awali. Kanuni hizi zimepunguza gharama ya uogeshaji kwa asilimia 90.

(ii) Kutungwa kwa Kanuni ya Utoaji wa Chanjo **(Vaccine and Vaccination)** 2020 GN No.180. Kanuni hii imeweka usimamizi thabiti wa usambazaji na utoaji wa chanjo nchini na kuwezesha utoaji wa chanjo sahihi, kuondoa matumizi ya chanjo feki na zilizoisha muda wake wa matumizi, kudhibiti magonjwa na kupunguza vifo vya mifugo, Aidha, Kanuni hii imeweka bei elekezi ya chanjo za Kimkakati 13. Kama ifuatavyo

| Na | Aina Ya Chanjo | Bei Holela Field kwa Dozi | Bei Elekezi kuchanja kwa Dozi |
|---|---|---|---|
| 1 | Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) | 2,000 | 550 |
| 2 | Chambavu (Black quarter) | 1,000 | 800 |
| 3 | Kimeta (Anthrax) | 1,000 | 500 |
| 4.1 | Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa Ng'ombe | 1,000 | 800 |
| 4.2 | Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa mbuzi na kondoo | 1,000 | 500 |
| 5 | Kutupa Mimba (Brucellosis) | 2,000 | 1,500 |
| 6 | Mdondo (Newcastle disease) | 100 | 50 |
| 7 | Mapele Ngozi (Lumpy Skin Disease) kwa ng'ombe | 1,000 | 600 |
| 8 | Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) | 500 | 350 |
| 9 | Homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP) | 500 | 350 |
| 10 | Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) | 6,000 | 3,000 |
| 11 | Kichaa cha Mbwa (Rabies) | 5,000 | 1,500 |
| 12 | Ndigana Kali (ECF) | 30,000 | 17,000 |
| 13 | Homa ya Bonde la Ufa (RVF) | 1,000 | 700 |

**NB:** Kwa kutumia bei elekezi kuchanja mifugo yote kwa magonjwa ya kipaumbele Serikali itapunguza gharama kwa wafugaji kutoka shilingi **bilioni 482.4** hadi **shilingi bilioni 237** sawa na punguzo la **asilimia 51.**

(iv) Marekebisho ya Kanuni ya Tozo **(Animal and Animal Products Movement Control)** Amendment 2020 GN. No. 489A ambapo ada na tozo mbalimbali zimefanyiwa mapitio kama ifuatavyo: -

a) Tozo ya kusafirisha nyama ya ng'ombe nje ya nchi imepunguzwa kutoka **shilingi 150** hadi shilingi 100 kwa kilo;
b) Tozo ya kusafirisha nyama ya mbuzi na kondoo imepunguzwa kutoka **shilingi 100** hadi **shilingi 50** kwa kilo;
c) Uagizaji na uingizaji wa chakula cha mifugo nje ya nchi imepunguzwa kutoka **shilingi 20,000** hadi **shilingi 10,000** kwa tani;
d) Tozo ya uuzaji wa ng'ombe nje ya nchi umepunguzwa kutoka **shilingi 30,000** hadi **shilingi 25,000** kwa ng'ombe; na
e) Tozo ya uuzaji mbuzi na kondoo nje ya nchi imepungua kutoka shilingi **7,500** hadi **shilingi 5,000** kwa mfugo.

Aidha, katika kipindi cha Mwaka 2018/2019, Serikali ilifuta jumla ya **tozo 54** katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi na kwa Mwaka 2019/2020 jumla ya **tozo 85** zimepunguzwa viwango vya tozo ili kuleta unafuu kwa wananchi na kuchochea ushindani ndani na nje ya nchi.

(v) Kanuni ya Uhimilishaji Mifugo **(Artificial Breeding)** 2020 GN No.118, Kanuni hii imeweka usimamizi thabiti wa uhimilishaji mifugo nchini, kupunguza hasara na gharama za uhimilishaji kwa mfugaji na hivyo kuongeza kasi ya uboreshaji wa koosafu za mifugo ambapo pia imeweka **bei elekezi ya shilingi 10,000** badala ya shilingi zaidi ya **25,000** iliyokuwa ikitozwa kwa ng'ombe

(vi) Kanuni ya Utafiti ya Mifugo (Livestock Research Institute Regulation) 2020 GN. No. 462/2020. Kanuni hii imeweka wajibu kwa watafiti kufanya utafiti kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa katika Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti, Kuondoa uwezekano wa kufanya tafiti za nje ya nchi pekee, kupanua wigo wa tafiti kwa kuzitambua tafiti zinazofanywa na watafiti wengine nje ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) wakiwemo vijana wanaomaliza masomo ya Shahada ya Uzamili (Masters) na Shahada ya Uzamivu (PhD). Kuzikusanya pamoja tafiti na kusambaza matokeo ya utafiti kwa watumiaji (Beneficiaries). Katika mwaka 2019/2020 jumla ya **tafiti 433** zilikusanywa kupitia Kanzidata iliyoanzishwa na TALIRI ikilinganishwa na wastani wa **tafiti 11 tu** zilizokuwa zikikusanywa katika kipindi cha miaka ya nyuma; na

(vii) Kanuni ya Ukamataji wa Mifugo **(Impounded Animal) Regulation 2020.** Kanuni hii itaondoa ukamataji holela wa mifugo, imeweka wajibu kwa mkamataji kutoa taarifa kwa mamlaka na kuweka kumbukumbu za mifugo iliyokamatwa, kutoa huduma muhimu kwa wanyama kama maji, chanjo, malisho na tiba wanapokuwa wameshikiliwa na hivyo kupunguza vifo, wizi na kupotea. Pia, kanuni hii imetoa wajibu kwa wafugaji kutunza mifugo yao isiingie katika maeneo yasiyoruhusiwa kama Mashamba na Hifadhi. Kanuni hii itamaliza migogoro isiyoisha baina ya Wafugaji, Wakulima na Wahifadhi.

**4.0 UZALISHAJI WA MIFUGO NA MAZAO YAKE NA MIUNDOMBINU YA MASOKO**

**4.1 Huduma ya Uhimilishaji**

(i) Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2019/2020 jumla ya **ng'ombe 1,526,109** wamehimilishwa; na

(ii) Serikali imeandaa Kanuni za Uhimilishaji ambazo zimetoa bei elekezi ya kuhimilisha ng'ombe isiyozidi **shilingi 10,000** ikilinganishwa na gharama ya **shilingi 25,000** kabla ya kanuni hiyo.

**4.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba**

(i) Usambazaji wa mitamba katika Mashamba ya Serikali kwa mwaka umeongezeka kutoka **mitamba 11,449** mwaka 2015/2016 hadi **mitamba 18,255** mwaka 2019/2020.

**4.3 Uendelezaji Zao la Ngozi**

(i) Wakaguzi wa ngozi **113** wameteuliwa na wachunaji ngozi **735** wamejengewa uwezo; na

(ii) Serikali imeweka udhibiti wa utoroshaji na udanganyifu katika biashara ya ngozi kwa kutoza **asilimia 80** ya usafirishaji wa ngozi ghafi na **asilimia 10** ya usafirishaji wa ngozi zilizosindikwa kufikia hatua ya kati (wet blue) umeimarisha biashara ya ngozi nchini;

(iii) Serikali imejenga Kiwanda kipya cha Karanga chenye uwezo wa kuzalisha jozi na Soli za Viatu **1,200,000** kwa mwaka. Kuchakata ngozi futi za mraba **13,000,000** kwa mwaka pamoja na kuzalisha bidhaa mbalimbali za ngozi. Sehemu kubwa ya Ujenzi wa kiwanda cha kufuma Viatu imekamilika na tarehe **01/10/2020** uzalishaji wa viatu na bidhaa nyingine utaanza. Pia, baada ya miezi mitano (5) ijayo ujenzi na usimikaji wa mitambo na vifaa katika Kiwanda cha uchakataji wa ngozi utakamilika na kuanza uzalishaji. Aidha, jumla ya gharama za uwekezaji ni **shilingi bilioni 136** zitatumika, **"Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Mfuko wa Taifa wa Hifadhi za Jamii (PSSSF) na Jeshi la Magereza Tanzania kwa kuamua na kuridhia kujenga Kiwanda kikubwa cha mfano barani Afrika na maeneo mengine".**

(iv) Kwa upande wa Sekta Binafsi, Kiwanda cha ACE Leather Morogoro kinafanyiwa upanuzi mkubwa wenye thamani ya **shilingi bilioni 23** na ukarabati umekamilika kwa **asilimia 90.** Pia, ili kuongeza upatikanaji wa Machinjio bora, **Machinjio 30** za Kisasa zimejengwa na zinaendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali nchini ili kuwezesha uzalishaji na upatikanaji wa ngozi bora zitakazotumiwa na Viwanda kama malighafi; na

(v) Ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na zao la ngozi kwa mwaka 2019/2020 yameongezeka kutoka **shilingi bilioni 1.73** hadi **shilingi bilioni 9.1.**

Hatua zinazochukuliwa na Serikali zinalenga kumaliza changamoto za zao la ngozi ambapo

# MAFANIKIO SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

wananchi wamelalamika kwa muda mrefu juu ya ukosefu wa soko na bei nzuri ya zao hilo nchini ambapo wanauza kwa bei ya kutupa na nyingine kuoza na kutupwa, na nyingine kutelekezwa kwenye maghala. Vilevile, Taifa kutumia fedha za kigeni na gharama kubwa kuagiza viatu, pochi, mabegi, mikanda na bidhaa nyingine za ngozi kutoka nje ya nchi. Na wakati mwingine kuagiza bidhaa zilizotumika/zilizovaliwa yaani **MITUMBA** licha ya Taifa kuwa na mifugo mingi, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekataa kata kata mambo haya kuendelea na kwa muda mfupi ujao yatabaki kuwa historia.

**4.4 Udhibiti wa Biashara ya Mifugo na Mazao yake (Operesheni Nzagamba)**

Kabla ya Operesheni Nzagamba kulikuwa na ukwepaji mkubwa wa kulipa maduhuli ya Serikali yanayohusu biashara ya mifugo na mazao yake; uingizaji holela wa nyama, maziwa, mayai, vifaranga, madawa na vyakula feki au vilivyoisha muda wa matumizi toka nje ya nchi kinyume cha Sheria, Kanuni na Taratibu. Hali hii ilisababisha kukosekana kwa ushindani wa haki na kupelekea wazalishaji na viwanda vya ndani kufungwa, lakini pia ilihatarisha afya za walaji. Kupitia operesheni hiyo mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Kuongezeka mapato ya Serikali kutoka **Shilingi bilioni 9.5** mwaka 2015/2016 hadi **Shilingi bilioni 44.9** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 372.6**;
(ii) Kuongezeka kwa Viwanda vya kusindika nyama nchini kutoka **25** mwaka 2015 hadi viwanda **32** mwaka 2020 sawa na ongezeko la **asilimia 32**.;
(iii) Viwanda vya kusindika maziwa vimeongezeka kutoka **82** mwaka 2015 hadi 99 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia **21.** Pia, Kiwanda kipya cha Maziwa cha **GALAXY FOOD AND BEVERAGE COMPANY LIMITED** kina uwezo wa kusindika maziwa lita 75,000 kwa siku.

(iv) Kujengwa kwa Viwanda vipya vya kimkakati ikiwemo **TANCHOICE Company Limited** kilichopo Kibaha Mkoa wa Pwani chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe **1,000** na mbuzi/kondoo **6,000** kwa siku, ujenzi umekamilika na uzalishaji umeanza na tayari wameanza kuuza nyama katika masoko ya **OMAN** na **KUWAIT**. Gharama ya ujenzi wa Kiwanda hicho ni **shilingi bilioni 44**; Kiwanda cha **ELIA FOOD OVERSEAS LIMITED** Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe **500** na mbuzi/kondoo **4,000** kwa siku na thamani yake ni **shilingi bilioni 21**. Ujenzi umekamilika na uzalishaji utaanza wakati wowote kuanzia sasa; Kiwanda cha **BINJIANG COMPANY LIMITED** – Shinyanga chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe **1,000** kwa siku na ujenzi umeshakamilika ambao umegharimu jumla ya **shilingi bilioni 5.5**; na **Machinjio ya Kisasa ya Vingunguti** yenye uwezo wa kuchinja ng'ombe **2,000** na mbuzi/kondoo **4,000** kwa siku chenye thamani ya **shilingi bilioni 12.5**.

Viwanda hivi **vinne (4)** vya nyama ambavyo vimegharimu jumla ya **shilingi bilioni 83** vyenye uwezo wa kuchinja **ng'ombe 5,500** na **mbuzi/kondoo 14,000** kwa siku, ambapo ujenzi wake kwa sehemu kubwa umeshakamilika vitawezesha Taifa kuuza nyama nje ya nchi kwa kiasi kikubwa kuliko ilivyo sasa, kutatua tatizo la ukosefu wa soko la mifugo ambapo hivi sasa hulazimika kuuza mifugo hai katika nchi jirani, kuongeza ajira kwa vijana na upatikanaji wa fedha za kigeni na kukuza uchumi wa nchi;

(v) Serikali imerejesha umiliki wa Machinjio ya Dodoma kutoka kwa mwekezaji, Kampuni ya NICOL, baada ya kushindwa kuyaendesha kwa ufanisi na kusababisha uchakavu wa mitambo, madeni, na hivyo kusababisha hasara na kushindwa kutoa gawio kwa Serikali kwa kipindi cha miaka **11**. Mnamo tarehe 27 Disemba 2019, Wizara ilirejesha machinjio hayo kwa Serikali ambapo idadi ya ng'ombe wanaochijwa kwa siku wameongezeka kutoka wastani wa ng'ombe **41** hadi ng'ombe **150**. Pia, kwa kipindi cha miezi sita baada ya machinjio kurejeshwa chini ya usimamizi wa Serikali, yameweza kutoa gawio la shilingi **milioni 70** kwa Serikali.

**5.0 RASILIMALI ZA MALISHO, VYAKULA NA MAJI KWA MIFUGO**

**5.1 Malisho, Vyakula vya Mifugo na Maji kwa ajili ya Mifugo**

(i) Serikali imeongeza maeneo ya malisho ya mifugo yaliyotengwa kutoka **hekta milioni 1.4** mwaka 2015/2016 hadi **hekta milioni 5** mwaka 2019/2020;
(ii) Kati ya mwaka 2015/2016 na 2019/20 viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo vimeongezeka kutoka **80** kufikia **105** vyenye uwezo wa kuzalisha **tani 6,684** kwa siku na hivyo kupunguza uagizaji wa vyakula vya mifugo kutoka nje ya nchi; na
(iii) Jumla ya mabwawa **104** yamejengwa na kukarabatiwa katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo kupelekea kuwa na **mabwawa 1,482** katika mwaka 2019/2020 ikilinganishwa na mabwawa/malambo **1,378** mwaka 2015/2016.

**5.2 Utatuzi wa Migogoro Baina ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi**

Serikali katika jitihada za kupata suluhisho la migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imetekeleza yafuatayo: -

(i) **Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** aliamua kuunda Timu ya Mawaziri nane (8) na baadaye iliamuriwa kufuta baadhi ya maeneo ya Hifadhi za Misitu, Maeneo Tengefu na Mashamba ya Serikali na kuagiza yagawiwe kwa wananchi kwa ajili ya mifugo, kilimo na makazi. Pia, iliamriwa kuwa **Vijiji 920** vilivyoanzishwa ndani ya Hifadhi virasimishwe na wananchi waendelee kuyatumia maeneo hayo kwa ajili ya mifugo na matumizi mengine.

Pia, iliamuriwa kuwa wananchi wanaoishi eneo la wazi ndani ya **mita 500** katika mipaka ya Hifadhi **(Buffer zone)** wasihamishwe. Vilevile, wananchi wameruhusiwa kutumia eneo la **mita 60** kutoka katika kingo za mito kwa mwongozo ulioandaliwa.

(ii) Wizara imemega maeneo yenye ukubwa wa **hekta 29,428.49** katika Mashamba na Ranchi za Taifa na kuwapatia wananchi maeneo hayo kwa ajili ya shughuli za ufugaji na kilimo;
(iii) Viongozi wa Wizara wamefanya ziara katika Halmashauri **152** zenye mifugo ili kusikiliza, kutoa elimu na kutatua migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ambapo jumla ya migogoro **304** imetatuliwa kupitia ziara hizo;
(iv) Wizara katika kuhakikisha wafugaji wanapata maeneo ya malisho imetenga na kuwapangisha wafugaji kwa muda wa mwaka mmoja mmoja jumla ya h**ekta 78,470.97** kutoka kwenye taasisi zake; na
(v) Wizara imeunda Timu ya Wataalam kushughulikia Migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ambayo inahusisha Ofisi ya Rais, OR-TAMISEMI, Wizara za Mifugo, Kilimo, Ardhi; Mambo ya Ndani, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa kiasi kikubwa Timu hii imetatua migogoro mingi.
(vi) Wizi wa mifugo umepungua nchi baada ya Wizara kufanya ufuatiliaji wa mtandao wa wizi wa mifugo katika mikoa ya Arusha, Rukwa, Katavi, Mara, na Tanga ambapo njia mbalimbali za wizi wa mifugo zilibainishwa. Wizara imeweka mikakati ya kudhibiti ya kutokomeza wizi wa mifugo nchini ikiwa ni pamoja na: (1) kuunda kanda saba (**7**) za doria za kudhibiti wizi wa mifugo; (2) kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama vya maeneo husika kuwabaini na kuwatia nguvuni wezi wote wa mifugo; na (2) kuweka alama za utambuzi wa mifugo.

Hatua hizi zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano zimepunguza migogoro ya wafugaji, wakulima, wahifadhi na watumiaji wengine wa ardhi kwa kiasi kikubwa ambapo kwa kiasi fulani maeneo ya malisho yameongezeka. Pia, kupigana na kuuana baina ya wafugaji na wakulima kumepungua, matukio ya mifugo kuwekewa sumu na kukatwa mapanga yamepungua tofauti na ilivyokuwa zamani. Elimu inaendelea kutolewa na ushirikiano unazidi kuimarika.

**6.0 HUDUMA ZA AFYA YA MIFUGO**

**6.1 Magonjwa ya Mifugo**

(i) Majosho mapya **104** yamejengwa na majosho **542** yamekarabatiwa katika kipindi cha Mwaka 2018/2019 na Mwaka 2019/2020 pamoja na kutolewa dawa za ruzuku za kuogesha mifugo katika majosho yote yanayofanya kazi nchini;
(ii) Michovyo ya kuogesha mifugo imeongezeka kutoka michovyo **19,988,280** mwaka 2015/2016 hadi michovyo **251,389,517** mwaka 2019/2020;
(iii) Maambukizi ya magonjwa ya mifugo yamepungua kwa **asilimia 29** na vifo vya mifugo vimepungua kwa **asilimia 37**; na
(iv) Uzalishaji wa chanjo kwa mwaka umeongezeka kutoka **dozi 26,367,200** mwaka 2015/16 hadi **dozi 58,016,325** mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 120.
(v) Mpango wa kuanza ujenzi wa kliniki na maabara kwa kila Halmashauri umeanza ambapo tayari maabara **moja** (**1**) imejengwa na inafanya kazi.

**6.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Chanjo**

(i) Wizara imeandaa utaratibu wa manunuzi ya pamoja (bulk procurement) ya chanjo na bei elekezi ili kuongeza upatikanaji wa chanjo, kulinda ubora wa chanjo na kupunguza gharama ya chanjo kwa wafugaji; na

(ii) Ujenzi wa kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha chanjo za mifugo aina 37 cha Hester Bioscience Africa Limited – Kibaha mkoa wa Pwani umekamilika kwa asilimia 90. Kiwanda hiki kitazalisha **dozi bilioni 1.5** kwa mwaka kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Thamani ya Kiwanda hicho ni **shilingi bilioni 44**.
(iii) Pia, Kituo cha Uzalishaji wa chanjo cha Kibaha (TVI) kinapanuliwa ili kuweza kuzalisha **chanjo zote za kimkakati 13,** hivi sasa Kituo hiki kinazalisha chanjo **sita (6)** tu na chanjo **saba (7)** zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Jitihada hizi za Serikali zitaifanya nchi yetu isiagize chanjo za Mifugo kutoka nje ya nchi, kurahisisha upatikanaji na unafuu wa bei ya chanjo, kudhibiti magonjwa na kuokoa fedha za kigeni zilizokuwa zinatumika kuagiza chanjo kutoka nje ya nchi.

**7.0 UTAFITI, MAFUNZO NA UGANI**

**7.1 Utafiti wa Mifugo**

(i) Wizara, imeandaa Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mifugo ya miaka mitano (Livestock Research agenda 2020 -2025).
(ii) Wizara imeimarisha Kituo cha Uhawilishaji Kiinitete (MOET) Mpwapwa kwa kukipatia vitendea kazi mbalimbali. Aidha, jumla ya **viinitete 34** vimevunwa na kupandikizwa kwa ng'ombe waleaji **mimba 34.**

**7.2 Mafunzo ya Mifugo na Ugani**

(i) Idadi ya wanachuo wanaodailiwa kwa mwaka imeongezeka kutoka **2,082** mwaka 2015/2016 hadi **3,642** mwaka 2019/2020.
(ii) Kati ya mwaka 2015/2016 na 2019/2020 jumla ya wafugaji **20,027** na Wagani **822** wamepatiwa mafunzo mahsusi kuhusu ufugaji bora wa kibiashara ikiwemo uzalishaji mifugo, udhibiti wa magonjwa ya mifugo, ujasiriamali na mbinu za masoko.

**SEKTA YA UVUVI**

**8.0 Sera, Sheria na Kanuni**

Serikali imefanya mapitio na kuboresho Sheria, Kanuni, mipango na tozo mbalimbali zinazosimamia Sekta ya Uvuvi ili ziweze kuwa rafIki kwa watumiaji na hivyo kupunguza vitendo vya ukiukwaji wa sheria na kanuni za uvuvi kwa uendelevu wa rasimali za uvuvi. Sheria na Kanuni zilizotungwa na kufanyiwa marekebisho ni kama ifuatavyo:-

i. Kutungwa kwa Sheria Mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu ya Mwaka 2020 (The Deep-Sea Fisheries Management and Development Act, 2020) na kufuta Sheria iliyokuwepo (Deep Sea Fishing Authority Act; No.1 ya Mwaka 1998) ili kuimarisha mapambano dhidi ya uvuvi haramu na kuweka vivutio ili kuvutia uwekezaji na uvuvi katika ukanda wa uchumi wa bahari kuu;

ii. Kufumua Sheria ya Uvuvi Na.22 ya Mwaka 2003 ili kuandaa Sheria mbili zinazotenganisha masuala ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji kwa lengo la kuondoa mapungufu/kasoro zilizopo ili kukidhi mahitaji ya sasa; na
iii. Kuandaa Agenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji (The Fisheries and Aquaculture Research Agenda 2020 – 2025). Kanuni hii imeweka wajibu kwa watafiti kufanya utafiti kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa katika Ajenda ya Kitaifa ya Utafiti, Kuondoa uwezekano wa kufanya tafiti za nje ya nchi pekee, kupanua wigo wa tafiti kwa kuzitambua tafiti zinazofanywa na watafiti wengine nje ya TAFIRI wakiwemo vijana wanaomaliza masomo ya Shahada ya Uzamili (Masters) na Shahada ya Uzamivu (PhD). Kuzikusanya pamoja tafiti na kusambaza matokeo ya utafiti kwa watumiaji (Beneficiaries). Katika mwaka 2019/2020 jumla ya **tafiti 500** zilikusanywa kupitia Kanzidata iliyoanzishwa na

# MAFANIKIO SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

TAFIRI ikilinganishwa na wastani wa **tafiti 22** zilizokuwa zikikusanywa katika kipindi cha miaka ya nyuma.

iv. Serikali imefanya Marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 kupitia GN Na.492 ya Mwaka 2020 ili kuwezesha wazawa kushiriki kikamilifu katika shughuli za uvuvi, biashara ya samaki na mazao ya uvuvi pamoja na kuliwezesha Taifa kunufaika na rasilimali za uvuvi. Baadhi ya mabadiliko makubwa yaliyofanyika katika Kanuni mpya ni kama ifuatavyo:-

a) Kuruhusu matumizi ya **leseni moja** kwa eneo moja la uvuvi (Water body) badala ya kila Halmashauri;
b) Kuondoa ukomo wa **sentimita 85** katika kuvua samaki aina ya sangara;
c) Kuruhusu matumizi ya nyavu za dagaa **milimita 8** katika ukanda wa bahari badala ya **milimita 10**
d) Kuruhusu matumizi ya taa za nguvu ya jua (solar) katika maeneo ya mavuvi katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika;
e) Kuruhusu matumizi ya nyavu za makila za kuunganisha kufikia ukomo wa macho 78 katika Ziwa Victoria na macho 144 katika Ziwa Tanganyika uvuvi wa samaki aina ya Sangara na Migebuka;
f) Kuruhusu matumizi ya ringnet katika uvuvi wa dagaa Ziwa Tanganyika umbali mita 1,000 kutoka mwaloni, peninsula na kisiwa;
g) Kuruhusu nyavu za makila za ukubwa wa macho ya inchi 1.5 kwa ajili ya uvuvi wa samaki aina ya vitui na mantura katika Ziwa Nyasa;

h) Kuruhusu tofauti ya kipimo (Standard error) kisichopungua sentimita 2 kwa samaki wabichi na sentimita 3 kwa samaki waliokaushwa kutoka katika kipimo kilichokubalika kisheria kwa samaki aina ya Sangara;

i) Kuruhusu misimu ya uvuvi wa samaki aina ya Kambamiti katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Machi hadi tarehe 30 Septemba kwa Kanda ya Kaskazini (Bagamoyo na Pangani) na kuanzia tarehe 1 Aprili hadi tarehe 31 Agosti ya kila mwaka kwa Kanda ya Kusini (Kisiju-Mkuranga, Rufiji na Kilwa);

j) Kuruhusu uuzwaji wa Pweza wenye uzito kuanzia **gramu 440** badala ya **gramu 500** baada ya kuchakatwa;

k) Kuruhusu uvuvi wa Kambakoche aina ya Pakupaku (Sandy lobster) kuanzia gramu 250 badala ya **gramu 500;**

l) Kuruhusu kuvuliwa kwa samaki jamii ya Perege wenye urefu kuanzia **sentimita 20** katika Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu badala ya **sentimita 25**;

m) Kuruhusu samaki wasiochakatwa (whole fish) waliotolewa matumbo kuuzwa katika masoko ya Kikanda na Kimataifa;

n) Kuruhusu biashara ya mabondo chini ya urefu wa sentimita 12 au uzito wa gramu 13 kwa mabondo mabichi na urefu wa sentimita 8 au uzito wa gramu 4 kwa mabondo makavu; na

o) Kuweka miongozo ya usimamizi wa uvuvi katika maji madogo kwenye maziwa ya Eyasi, Manyara, Kitangiri, Rukwa, Singidani, Basuto, Burigi na bwawa la Bahi na mto Kilombero.

v. Serikali imepunguza viwango vya tozo na ada katika uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi ili kupunguza gharama na kuhimili ushindani wa kibiashara ndani na nje ya nchi. Baadhi ya maeneo ambayo viwango vimepunguzwa ni kama ifuatavyo:-

a) Tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi toka Ziwa Tanganyika imepungua kutoka **Dola za Marekani 1.5** hadi **Dola za Marekani 0.5** kwa kilo;
b) Tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kwa dagaa wa bahari na Ziwa Nyasa kutoka **Dola za Marekani 1** hadi **Dola za Marekani 0.16;**
c) Ada ya Leseni ya kusafirisha dagaa nje ya nchi kwa wafanyabiashara wadogo imepungua kutoka **Dola za Marekani 1,000** hadi **Dola za Marekani 250** na kupungua kutoka **Dola za Marekani 1,800** hadi **Dola za Marekani 500** kwa Wafanyabiashara wakubwa**;**
**d)** Ada ya leseni ya mazao mengine ya bahari kama Pweza, Kambakoche na Kaa kupungua kutoka **Dola za Marekani 2,500** hadi **Dola za Marekani 500** kwa kilo kwa Wafanyabiashara wadogo na kupungua kutoka **Dola za Marekani 2,700** hadi **Dola za Marekani 1,000** kwa Wafanyabiashara wakubwa; na
e) Tozo ya usafirishaji wa samaki aina ya migebuka kwenda nje ya nchi imepungua kutoka **Dola za Marekani 0.5** hadi **Dola za Marekani 0.3** kwa kilo.

**8.0 Ujenzi wa miundombinu**

(i) Serikali imeimarisha mialo ya kisasa **13** ya kupokelea samaki na kuwa ya kisasa katika Ukanda wa Ziwa Victoria **6**; Ukanda wa Ziwa Tanganyika minne (**4**); katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi mitatu (**3**);
(ii) Soko la Samaki Feri (Dar es Salaam) limeimarishwa kwa kujengewa choo cha kisasa chenye **matundu 12**, mabafu nane (**8**), ofisi mbili (**2**) na stoo moja (**1**). Pia, Serikali imekamilisha kufanya Upembuzi Yakinifu wa kufanya ukarabati mkubwa wa Soko la Feri – Dar es Salaam ambapo awamu ya Kwanza imetengewa **shilingi bilioni 1.7**.
(iii) Miundombinu ya Soko la Samaki la Kasenda, Chato (Geita) imeimarishwa kwa kujengewa barabara ya kuingia sokoni kwa kiwango cha lami kutoka Muganza. Vilevile, ujenzi wa Soko la Samaki Nyakaliro, Sengerema (Mwanza) umekamilika; na
(iv) Serikali imeweka Mzani katika **Soko la Kimataifa Kirumba (Mwanza)** ambao umeondoa udanganyifu katika ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mapato ya Serikali. Pia, maandalizi ya kufanya ukarabati mkubwa katika Soko hilo yamekamilika ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 1.1** zitatumika.

**10.0 Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

(i) Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kupitia Mshauri Mwelekezi Kampuni ya M/S Sering Ingegneria ya nchini Italia kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.4;** na
(ii) Serikali ipo katika hatua za mwisho za mazungumzo na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa Bandari kwa mkopo kutoka Exim Bank ya Korea Kusini.

**11.0 Kuanza kwa Uvuvi wa Bahari Kuu**

(i) Serikali imefufua Shirika la TAFICO ambapo kazi mbalimbali zimefanyika ikiwemo uandaaji wa Mpango Biashara (Business Plan) wenye maeneo matatu makubwa yanayojumuisha miradi midogo kumi (10) yenye thamani ya jumla ya **shilingi 89,282,057,278.00** ikiwemo miradi ya uvuvi, kununua meli mbili (2) za uvuvi Long liner na Purse Seiner na miradi ya ukuzaji viumbe maji. Aidha, utambuzi na tathmini ya majengo na mali za shirika umefanyika. Vilevile, ukarabati wa majengo na miundombinu unaendelea;

(ii) Serikali imepata ufadhili kutoka Serikali ya Japan kupitia Programu ya Maendeleo ya Uchumi na Jamii - Japan (The Economic and Social Development Programme) wenye thamani ya kiasi cha **shillingi bilioni 4.2** ambapo sehemu ya fedha hizo itatumika katika ujenzi wa meli yenye urefu wa mita 18 itakayovua katika maji ya kitaifa. Aidha, Msaada huo utahusisha usimikaji wa mtambo wa kuzalisha barafu na ujenzi wa ghala la baridi la kuhifadhia samaki (Cold room).

(iii) Serikali ipo katika hatua za mwisho ili kuingia mkataba na Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo Duniani (IFAD) kwa ajili ya kupata mkopo wenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 68.8** ambazo zitatumika kununua meli Uvuvi wa Bahari Kuu aina ya Longliner, Kujenga kiwanda cha Kuchakata samaki, kujenga kiwanda cha kutengeneza vyakula bora vya samaki, na kuweka miundombinu wezeshi ya kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa.

**12.0 Uzalishaji wa mazao ya uvuvi kwenye maji ya asili**

(i) Kuongezeka kwa wingi (biomass) wa samaki katika maji yetu hususan katika Ziwa Victoria ambapo samaki aina ya Sangara wameongezeka kutoka tani **417,936** mwaka **2016** hadi tani **816,964** mwaka 2020, sawa na ongezeko la **asilimia 95.5** na urefu wa Sangara umeongezeka kutoka wastani wa **sentimeta 16** hadi **sentimeta 25.2**. Aidha, dagaa wameongezeka kutoka tani **660,333** mwaka 2017 hadi kufikia tani **936,247** mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 41.8**. Aidha, mafanikio mengine ni pamoja na kupungua kwa samaki wachanga aina ya Sangara wenye urefu wa chini ya **sentimita 50** kutoka **asilimia 96.6** mwaka 2017 hadi kufikia **asilimia 62.8** mwaka 2019; kuongezeka kwa samaki aina ya Sangara wenye urefu wa kuanzia **sentimeta 50** hadi **85** kutoka **asilimia 3.3** mwaka 2017 hadi kufikia **asilimia 32** mwaka 2019; na kuongezeka kwa samaki aina ya Sangara wenye urefu wa juu ya **sentimenta 85** kutoka **asilimia 0.4** mwaka 2017 hadi kufikia **asilimia 5.2** mwaka 2019;

(ii) Kuongezeka kwa uzalishaji/uvunaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani **362,645** zenye thamani ya **shilingi trilioni 1.48** mwaka 2015/2016 hadi **tani 497,567** za samaki zenye thamani ya **shilingi trilioni 2.34** hadi Mwezi Juni mwaka wa fedha 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 37.2**;

(iii) Kuongezeka kwa mauzo ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka mauzo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 379.25** mwaka 2015/2016 hadi **shilingi bilioni 692** mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la **asilimia 82.5**;

(iv) Kupungua kwa uingizaji wa samaki kutoka nje ya nchi kutoka samaki wenye thamani ya **shilingi bilioni 56.12** mwaka 2016/2017 hadi **shilingi bilioni 0.16** mwaka 2020 sawa na upungufu wa **asilimia 99.7**. Hivyo, kusaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, kusaidia kulinda soko la ndani, kuongeza ajira na kupunguza ulali wa kibiashara; na

(v) Kuongezeka kwa mapato kutoka shilingi **bilioni 17.8** mwaka 2015/2016 **hadi shilingi bilioni 33.7** mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la **asilimia 89.3.**

**13.0 Usindikaji na Usafirishaji wa minofu ya samaki na mazao mengine ya uvuvi**

(i) Usindikaji wa minofu ya samaki aina ya Sangara umeongezeka kutoka **tani 23,000.58** mwaka 2015/2016 hadi **tani 39,748.37** mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la **asilimia 72.6**; na

(ii) Huduma za usafirishaji wa mazao ya uvuvi kwenda masoko ya Ulaya umeboreshwa ambapo viwanja vya Ndege vya ndani ya nchi vya Mwanza, KIA na JKIA-Dar es Salaam vimeanza kutumika kusafirisha mazao hayo moja kwa moja kutoka nchini badala ya kupitia kwenye viwanja vya nchi jirani. Hali hii imepunguza ucheleweshwaji wa usafirishwaji na gharama za usafirishaji wa minofu ya samaki kutoka **Dola za Marekani 3.8** hadi **Dola za Marekani 2.5** kwa kilo. Katika kipindi hiki, jumla ya **kilo 199,710.6** za mabondo na minofu ya Sangara zilisafirishwa kupitia viwanja vya ndege vya ndani.

**14.0 Ukuzaji wa Viumbe maji na Uzalishaji wa samaki katika Mabwawa na Vizimba**

(i) Uzalishaji na ukuzaji viumbe maji umeimarika, ambapo wakuzaji viumbe maji wameongeza kutoka **18,843** mwaka 2015 hadi kufikia **26,474** mwaka 2020**,** vilevile, uzalishaji umeongezeka kutoka **tani 3,112** mwaka 2015 hadi **tani 18,080** za samaki mwaka 2020. Aidha, tumeongeza idadi ya mabwawa kutoka **22,545** mwaka 2015 hadi **26,445**, Vizimba vya kufugia samaki (Fish cages) vimeongezeka kutoka **109** mwaka 2015

# MAFANIKIO SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI

hadi **431** mwaka 2020; na

(ii) Uzalishaji wa vifaranga vya samaki katika vitotoleshi vya Serikali na Sekta binafsi umeongezeka kutoka **8,090,000** mwaka 2015 hadi kufikia vifaranga zaidi ya **50,000,000** mwaka 2020**.** Kutokana na uzalishaji huo hivi sasa nchi yetu haiagizi vifaranga tena kutoka nje ya nchi.

**15.0 Kuimarisha huduma za ugani**

Serikali imeimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kwa kujenga madarasa na kumbi za kufundishia katika Kampasi za Mbegani Bagamoyo - Pwani; Nyegezi - Mwanza; Mtwara/Mikindani - Mtwara; Kibirizi - Kigoma na Gabimori – Mara ili kuongeza udahili wa wanachuo ambapo jumla ya wanachuo **5,249** walidahiliwa katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020; na Wadau **7,184** walipatiwa mafunzo rejea ya muda mfupi katika mbinu za kuvua na ukuzaji viumbe maji. Aidha, jumla ya vyama vya ushirika vya uvuvi **102** vimetambuliwa na vyama vipya **26** vimeanzishwa na hivyo kufanya vyama vya ushirika vya uvuvi vilivyo hai kufikia **128** katika kipindi cha miaka mitano (2015-2020). Pia, katika kipindi hicho Chama Kikuu Cha Ushirika Wa Wavuvi Tanzania (CHAKUWATA) kimeanzishwa.

**16.0 Kufanya na kutumia matokeo ya tafiti katika kuboresha shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji**

Wizara kupitia TAFIRI imeendela kufanya utafiti na kutumia matokeo ya tafiti hizo katika kuboresha shughuli za uvuvi, ukuzaji viumbe maji na biashara ya mazao ya uvuvi nchini.

Mafanikio hayo yamepatikana kupitia kazi mbalimbali ikiwemo: -

(i) Uanzishwaji wa Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji **(National Fisheries and Aquaculture Research Agenda 2020-2025).** Uwepo wa ajenda hiyo umesaidia katika kutoa mwongozo kwa Taasisi za umma na binafsi, vyuo na watafiti wengine kuzingatia vipaumbele vya Taifa katika tafiti za uvuvi na ukuzaji viumbe maji;

(ii) Uanzishwaji wa Kanzidata ya Tafiti za Uvuvi na Ukuzaji viumbe maji **(Database of Fisheries and Aquaculture Research)** ambao umesaidia kuweza kukusanya taarifa za tafiti za uvuvi na ukuzaji viumbe maji kutoka **tafiti 22** mwaka 2015 hadi **tafiti 500** mwaka 2020. Aidha, Kanzidata hiyo imeruhusu matumizi ya matokeo ya tafiti za wanafunzi wa Shahada za Uzamili na Uzamivu katika uendelezaji wa Sekta ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji; na

(iii) Utungaji wa Kanuni za kusimamia tafiti katika Tasnia ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji **(Fisheries and Aquaculture Research Regulations, 2020)** umesaidia katika kutoa miongozo ya namna ya kufanya tafiti, usambazaji wa taarifa za tafiti na matumizi ya tafiti hizo. Kanuni hizo hazikuwahi kuwepo katika miaka ya nyuma.

**17.0 Kuendelea kupambana na uvuvi haramu ili uwe uvuvi endelevu na wenye tija**

Serikali imefanikiwa kupambana na uvuvi haramu kwa kufanya mambo yafuatayo: -

(i) Kuongezeka kwa vituo vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi kutoka **27** mwaka **2016** hadi kufikia **32** mwaka 2020. Aidha, imeanzisha Kanda kuu tatu (**3**) **za Ziwa Victoria; Ziwa Tanganyika na Pwani.** Pia, imeanzisha Kanda ndogo tatu (**3**) za **Sengerema, Ukerewe na Simiyu-Magu** katika Kanda Kuu ya Ziwa Victoria ili kuongeza wigo wa usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi.

(ii) Kufanya Operesheni Maalum za Kikanda (Sangara 2018, Jodari na NMATT) na doria na kupelekea kuondoa zana haramu zilizokuwa zikitumika katika maeneo ya uvuvi na kuwezesha kupungua kwa uvuvi haramu na biashara haramu ya mazao ya uvuvi kwa asilimia **80** katika maji baridi na kupungua kwa uvuvi haramu wa kutumia mabomu na milipuko mingine kwa **asilimia 100** katika Mwambao wa Bahari ya Hindi.

(iii) Doria zimeendelea kufanyika ambapo jumla ya vipande **1,271,468** vya nyavu haramu vimekamatwa na kuteketezwa kwa moto; mabomu **4,583** yalikamatwa na watuhumiwa **14,384** walikamatwa na kutozwa faini na wengine kufikishwa mahakamani

**18.0 Kujenga viwanda vya kusindika, kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi, zana za uvuvi na chakula cha samaki**

Serikali imehamasisha sekta binafsi ili kuwekeza katika viwanda vitano **(5)** vya kutengeneza nyavu, viwanda viwili (**2**) vya kutengenza boti. Aidha, Serikali imehamasisha Sekta binafsi kujenga maghala ya kuhifadhia/kugandisha samaki na mazao yake kutoka **maghala nane** (**8**) yenye uwezo wa kuhifadhi **tani 31** mwaka 2015 hadi kufikia **maghala 90** mwaka 2020 yenye uwezo wa kuhifadhi wastani wa **tani 350** kwa siku. Vilevile, viwanda vikubwa vya kuchakata samaki vimeongezeka kutoka **15** mwaka 2015 hadi **19** mwaka 2020. Viwanda vya kati vya uchakataji samaki vimeongezeka kutoka viwanda vitatu (**3**) mwaka 2015 hadi vitano (**5**) mwaka 2020 na viwanda vidogo vimeongezeka kutoka **11** mwaka 2015 hadi **33** mwaka 2020. Aidha, Kiwanda kimoja cha kuchakata Pweza kimejengwa katika Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani. Pia, juhudi za kufufua viwanda viwili (**2**) vilivyofungwa mkoani Mwanza na Mara zinaendelea. Vilevile, katika kipindi cha miaka mitano (5) Viwanda vipya **saba (7)** vya kuchakata mabondo vimejengwa.

**19.0 UKUSANYAJI WA MADUHULI**

Wastani wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Sekta za Mifugo na Uvuvi umeongezeka kutoka shilingi **bilioni 21** mwaka 2015 hadi kufikia **bilioni 72** mwaka 2018/2019 na shilingi **bilioni 74** mwaka 2019/2020, ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 252.4.**

**20.0 USHIRIKI NA UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI**

Wizara kupitia **Dawati la Sekta Binafsi** lililopo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi limewaunganisha wadau wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi katika kupata huduma mbalimbali ikiwemo kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili kupata huduma za mikopo, bima na hifadhi za jamii, kushiriki utatuzi wa changamoto za kibiashara za wadau kwa kuwaunganisha na taasisi na mamlaka zingine za Serikali kama vile TRA, TBS, TMDA, Wizara, Halmashauri, n.k. Aidha, Dawati la Sekta Binafsi limekuwa likitoa ushauri wa kitaalam kwa wafanyabiashara katika maeneo yao ya uwekezaji na ujasiriamali. Baadhi ya mafanikio ni kama ifuatavyo: -

(i) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi kutoka Benki za TADB (bilioni **30**), NMB (bilioni **30**) na CRDB (bilioni **4.2**) yenye jumla ya kiasi cha **shilingi bilioni 64.3** mwaka 2020. Kipindi cha nyuma hapakuwepo na mikopo iliyotolewa na benki hizo katika sekta husika;

(ii) Kuwezesha kampuni ya Taifa ya Bima (NIC), Jubilee, na Reliance kukubali kutoa bima kwa mikopo ya wafugaji na wavuvi. Aidha, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (PSSSF) limekubali kutoa hifadhi za jamii kwa wafugaji na wavuvi;

(iii) Jumla ya wadau **234** wamefika na kuhudumiwa kwa masuala mbalimbali ikiwemo utatuzi wa changamoto za kibenki, masoko, uwekezaji na usafirishaji, kuanzishwa kwa miradi na viwanda vipya **41** na kufufua jumla ya miradi na viwanda **6** vilivyokuwa havifanyi kazi;

(iv) Kuwezesha kufufuliwa kwa Kiwanda cha Samaki cha Migebuka Fisheries Ltd baada ya kupata mwekezaji mpya, Kampuni ya ALPHA Tanganyika Flavour Ltd;

(v) Serikali inaendelea kufanya tathmini ya kodi na tozo ambazo zinalalamikiwa na wadau, ambapo kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha 2020 ilipelekea kufutwa kwa kodi nane (**8**) katika ununuzi wa vifaa na zana za Ukuzaji Viumbe Maji. Aidha, jumla ya tozo **85** za mifugo na uvuvi zimepunguzwa viwango katika mwaka 2020 na kuleta unafuu mkubwa kwa wadau; na

(vi) Serikali imefanikisha kuandaliwa kwa Mipango ya Biashara (Business Plan) kwa Taasisi za Wizara ambazo ni NARCO, TALIRI, LITA, TVLA na TAFICO na mchakato wa kupata mikopo upo katika hatua mbalimbali. Aidha, Taasisi hizi hazikuwahi kuwa na mipango ya biashara huko nyuma.

**21.0 HITIMISHO**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu napenda kutolea ufafanuzi baadhi ya mambo muhimu kuhusiana na Kanuni mpya za Uvuvi na Mifugo za Mwaka 2020 kama ifuatavyo

(i) Katazo la matumizi ya jenereta kama chanzo cha mwanga katika uvuvi wa bahari kama ilivyoainishwa katika **Kanuni ya 66(1)(gg)** kwa kuwa utafiti wa chanzo cha mwanga baharini haujakamilika hivyo nimeruhurusu matumizi ya jenereta katika uvuvi wa Bahari hadi Disemba 31, 2020; na

(ii) Mabadiliko ya nyavu za makila kwa ajili ya uvuvi wa samaki ukanda wa Bahari ya Hindi kubadilika kutoka **inchi 1.5 hadi inchi 3 Kanuni ya 66(1)(f)** kwa kuwa ubadilishaji wa nyavu unahitaji muda na kwa kuwa wavuvi walikuwa na nyavu za nchi 1.5 ambapo zilikuwa zinaruhusiwa kwa mujibu wa Sheria hivyo ninaruhusu matumizi ya nyavu hizo hadi tarehe **31 Disemba, 2020** ili kutoa muda kwa wavuvi kubadilisha nyavu zao.

(iii) Kutozwa vibali vya ukaguzi na usafirishaji wa mifugo ndani ya nchi zaidi ya mara moja kwa mtu mmoja nimepokea malalamiko ya wafanyabiashara wa mifugo wanaonunua mifugo na kupeleka katika minada ya Upili ya Kizota Dodoma na Pugu Dar es Salaam na sehemu zingine nchini ambao hununua mifugo kwa lengo la kwenda kuchinja katika machinjio mbalimbali lakini kabla ya kufanya hivyo hulazimika kupita minada ya Upili kwa ajili ya ukaguzi kutimiza matakwa ya Sheria wanadai kuwa wanapolipia kibali cha kusafirisha mifugo (Movement Permit) kutoka kwenye minada ya awali kwenda minada ya upili wanalipia na kutoka mnada wa upili kwenda machinjio wanalipia kibali kipya kwa jina hilo hilo pamoja na kwamba hakuna mnunuzi mpya hivyo hapa **natoa mwongozo kuwa** Wafanyabiashara hao wasitozwe vibali vya kusafirishia mifugo mara mbili (Animal and Animal Pruducts Movement Control Amendments Regulations, 2020) Kanuni ya 6.

Katika kuhitimisha hotuba yangu nipongeze Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kwa jinsi ilivyo karibu na Wavuvi na Wafugaji kwa kutoa mafunzo, kuwaandaa kuwa na sifa za kukopesheka na kuwapatia mikopo katika vyama vyao vya ushirika na mtu mmoja mmoja tofauti na miaka ya nyuma ambapo wavuvi na wafugaji walidharaulika na kuambiwa ni watu wasiokopesheka lakini katika Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewezekana.

Pia nampongeza Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Abdalah Ullega, Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwani mafanikio haya bila ninyi yasingewezekana.

Kutokana na mafanikio makubwa niliyoyataja hapo juu, ni dhahiri kabisa kuwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, imefanya kazi kubwa ya kuleta mageuzi makubwa katika Sekta za Mifugo na Uvuvi nchini. Aidha, mageuzi haya yameleta faida kubwa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Vilevile, mafanikio yaliyopatikana yameweka msingi imara katika kuziendeleza Sekta hizi, na kuiwezesha nchi kufikia azma ya kuwa na uchumi wa viwanda, kuongeza fedha za kigeni na ajira, kuondoa umasikini, kukuza uchumi na kuongeza mapato ya Serikali.

Niwapongeze watanzania wote wakiongozwa na Jemedari wetu **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kufanikisha kuiwezesha nchi yetu kuingia katika uchumi wa kati ndani ya miaka **mitano (5)** badala ya **miaka 10** iliyotarajiwa na hivyo kulifanya Taifa letu kuwa gumzo kila kona duniani.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

# WACHEZAJI 10 WENYE UWIANO BORA WA USHINDI KARNE YA 21

**MUNICH,** Ujerumani

MWISHO wa siku soka ni kama mchezo mwingine wowote ambao unahusu ushindi. Jambo bora zaidi ni kushinda mchezo kila wiki, bila kujali mpinzani wako ni wa daraja la pili au ni moja ya timu bora duniani.

**Wakati wengi wakiwa na mtazamo huo, ni wachezaji wachache wenye vipaji muhimu na maadili ya kazi yao na kushinda kwa kipindi kikubwa cha muda. Wachezaji kama Lionel Messi na Cristiano Ronaldo mara kwa mara wamekuwa wakipongezwa kwa sifa yao ya kushinda.**

Makala haya yanakuchambulia wachezaji 10 wenye uwiano bora wa ushindi katika karne ya 21, sasa wafahamu...

### #10. THOMAS MULLER | 73.6% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

Ni mchezaji ambaye hatabiriki uwanjani, Thomas Muller amekuwa mtumishi mzuri wa Bayern Munich tangu alipoanza kuichezea kwa mara ya kwanza mwaka 2008.

Ni straika mwenye uwezo wa kutengeneza na kufunga bao na kutafuta nafasi nzuri. Muller ni mmoja wa washambuliaji bora kabisa kwenye kizazi chake. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ujerumani anaweza kucheza kama straika, mshambuliaji wa pili, winga zote na pia kama kiungo mshambuliaji.

Muller mwenye umri wa miaka 30, amecheza jumla ya mechi 533 katika mashindano yote kwa Bayern Munich, akifunga mabao 199 na kutoa pasi za mwisho 193.

### #9. TRENT ALEXANDER-ARNOLD | 73.9% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

Tayari ni mmoja wa beki bora wa kulia duniani, Trent Alexander-Arnold kuchomoza kwake kumekuwa kwa kuvutia.

Mhitimu wa akademi ya Liverpool aliichezea klabu hiyo mechi yake ya kwanza mwaka 2016, na hajaangalia tena nyuma tangu wakati huo. Ni mbunifu wa kutengeneza pasi na wengi wamekuwa wakisema kwamba, Alexander-Arnold anaweza kucheza safu ya kiungo kwa klabu na nchi yake kwa sababu ya aina ya uwezo alionao.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 21, amekuwa ni mmoja wa mabeki ambao watasaidia zaidi mashambulizi kwa Liverpool. Beki huyu wa timu ya Taifa ya England amecheza jumla ya mechi 134 katika mashindano yote kwa Liverpool hadi sasa.

### #8 EDERSON MORAES | 74% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

Katika kikosi cha Manchester City kina nyota wengi, lakini kiwango cha golikipa Ederson Moraes mara kwa mara hakiangaliwi.

Manchester City wailipa Benfica euro milioni 40 mwaka 2017 kwa saini ya Ederson, na haraka akachukua nafasi ya Claudio Bravo pale kwenye lango la klabu hiyo. Kipa huyo wa kimataifa wa Brazil ni mlinda mlango wa kisasa, mzuri kwa mipira yote. Mara kwa mara ni Ederson ndiye anayeanzisha mashambulizi ya Manchester City kutokana na uwezo wake wa kutengeneza pasi.

Wakati akiwa amefanya makosa machache katika msimu uliopita, lakini ubora wake hauwezi kuacha kuutaja. Katika umri wa miaka 26, bado hajawa kwenye kiwango cha juu. Ederson amecheza mechi 144 katika mashindano yote kwa Manchester City.

### #7. DAVID ALABA | 74% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

David Alaba amekuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga kwa muda sasa.

Ni muhitimu wa akademi ya Bayern Munich, Alaba ni mchezaji aliyejaliwa kipaji. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Austria anaweza kucheza kama mlinzi wa kushoto, mlinzi wa kati, kiungo na winga. Uwezo wake wa na ubunifu wa pasi, umekuwa ni mzuri sana bila ya kujali anacheza katika nafasi gani.

Nyota huyu mwenye umri wa miaka 28, amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake pale Bayern Munich na amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Barcelona, Real Madrid, Chelsea, Juventus na Manchester City. Tangu alipoanza kuichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza mwaka 2010, Alaba amecheza mechi 384 katika mashindano yote kwa Bavaria hao.

### #6. THIAGO | 74.6% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

Mmoja wa viungo bora duniani, Thiago amekuwa mchezaji muhimu zaidi kwenye kiungo ya Bayern Munich.

Nyota huyu wa kimataifa wa Hispania, alijiunga na Bayern Munich kutoka Barcelona mwaka 2013 kwa ada ya euro milioni 25. Huku akiwa anasumbuliwa na majeraha mara kadhaa, kiungo huyu amekuwa nguzo ya mafanikio ya Bayern kwa miaka.

Kama ilivyo kwa Alaba, Thiago amebakiwa na mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake na Bayern Munich. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 29, amekataa kusaini mkataba mpya, huku Liverpool wakitajwa kumuwania. Amecheza mechi 233 katika mashindano yote kwa Bayern Munich.

### #5. ADRIEN RABIOT | 75.6% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

Wakati Adrien Rabiot anaweza kuwa si mchezaji rahisi kukabiliana naye nje ya dimbani, lakini ubora wake unajulikana.

Zao la vijana kutoka pale Paris Saint-Germain, amecheza zaidi ya mechi 200 kwa mashindano yote na klabu hiyo, Rabiot aliamua kuhamia Juventus kwa uhamisho huru kipindi cha majira ya joto kilichopita. Baada ya mwanzo wa taratibu, nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, amekuwa nguzo ya safu ya kiungo kwa Juventus hasa kwa ubora wake na uwezo wa kutengeneza pasi.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ufarasa, ambaye alihusishwa na Everton na Manchester United Januari baada ya kuanza vibaya kule Juventus, sasa anaonekana kuimarika. Rabiot amecheza mechi 37 katika mashindano yote kwa Juventus msimu uliopita, akifunga bao moja.

### #4. NEYMAR | 76.3% YA MICHEZO YOTE ILISHINDA

Mmoja wa wachezaji bora duniani kwa sasa, Neymar pengine anafurahia msimu bora zaidi akiwa na Paris Saint-Germain.

Miamba hao wa Ligue 1 waliamua kutumia euro milioni 222 kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kutoka Barcelona, na kumfanya kuwa mchezaji ghali zaidi wa wakati wote katika historia ya usajili. Baada ya kuanza kwa kuwa majeruhi, Neymar sasa anaonekana kwenye ubora wake.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 28, amekuwa na wakati mzuri kucheza kwa upatina na Kylian Mbappe. Neymar amecheza jumla ya mechi 83 katika mashindano yote tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2017, akifunga mabao 70 na kutoa pasi za mwisho 40.

### #3. GABRIEL JESUS | 78.1% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

Wakati Gabriel Jesus hajawa katika kikosi cha kwanza cha Manchester City tangu alipojiunga na klabu hiyo, amekuwa na nyakati nzuri chini ya Pep Guardiola.

Jesus alijiunga na Manchester City kutoka Palmeiras mwaka 2017 kwa ada ya euro milioni 33. Straika huyo alinunuliwa kwa ajili ya kutoa ushindani kwa mkongwe Sergio Aguero, kitu ambacho ameshakifanya hadi sasa. Wakati Aguero ameendelea kuwa namba moja kwa Guardiola, Jesus mwenye umri wa miaka 23, amekuwa na rekodi nzuri ya kufunga mabao kwa klabu hiyo.

Uvumi umeenea kwamba raia huyo wa Brazil hana furaha katika klabu hiyo, huku Juventus na Inter Milan zote zikihusishwa na mchezaji huyo. Jesus amecheza mechi 152 katika mashindano yote kwa Manchester City, akifunga mabao 68.

### #2. JOSHUA KIMMICH | 78.2% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

Mchezaji wa mwisho wa Bayern Munich kwenye orodha hii ni mtu wao wa kazi, Joshua Kimmich.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ujerumani amekuwa mwenye kiwango kisichoshuka kwa Bavaria hao tangu alipojiunga nao. Kimmich alijiunga na Bayern Munich kutoka RB Leipzig mwaka 2015 kwa ada ya euro milioni 7. Kiungo huyo wakati wake akicheza kule Leipzig, alianza kama mlinzi wa kulia na sasa amejiimarisha pale Bayern Munich.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, anachukuliwa kama mlinzi bora zaidi wa kulia, huku kocha Hansi Flick pia akimtumia kwenye nafasi ya kiungo. Kimmich amecheza mechi 220 katika mashindano yote kwa Bayern Munich, na anaonekana atakuwa na majaliwa mazuri zaidi na timu hiyo.

### #1. PRESNEL KIMPEMBE | 78.9% YA MICHEZO YOTE ALIYOSHINDA

Mlinzi wa Paris Saint-Germain, Presnel Kimpembe ndiye mchezaji aliye na kiwango bora cha kushinda katika karne ya 2.

Ni zao la vijana pale Paris Saint-Germain, Kimpembe alianza kuichezea klabu hiyo mwaka 2014. Mlinzi huyu wa kati Kimpembe kwa sasa ndio chaguo la kwanza PSG.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, pia ni mshindi wa Kombe la Dunia, akiwa amelinyanyua na Ufaransa mwaka 2018. Kimpembe amecheza mechi 138 katika mashindano yote kwa klabu hiyo tangu mwaka 2014.



JESUS

## Nukuu

"Huo ni uongo. Sijapata ofa yoyote kwa sasa, mimi ndiye pekee mwenye jukumu la kuzungumzia majaliwa yangu," **Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger akikanusha taarifa kwamba amepewa ofa ya kuwa kocha mpya wa timu ya Taifa ya Uholanzi.**



"Nitachukua mwaka mmoja nje ya soka na nitajiuliza mwenyewe kama nitalimisi soka. Kama nikisema hapana, huo ndio utakuwa mwisho wa kazi ya ukocha kwa Jurgen Klopp, na kama siku moja sitakuwa tena kocha, ni kitu kimoja ndio nitakimisi: Ule muda wa tahayari kabla ya mchezo," **alisema Klopp akiiambia Sport Buzzer.**



"Anaweza kuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye Ligi Kuu ya England bila shaka yoyote, kwa sababu ana ubora na kipaji cha hali ya juu na mara zote akicheza huwa anawavutia wengi dimbani. Hivyo naamini atakuwa bora sana siku za usoni," **Willian aliyejiunga na Arsenal wiki moja iliyopita, akimtabiria makubwa mshambuliaji wa timu hiyo, Gabriel Martinelli.**









# TIMU ZAO ZIMESHUKA, WAPO SANA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KUNA msemo wa mashabiki wa soka usemao 'zinashuka timu tu, lakini wachezaji hawashuki'. Hili limeendelea kushamiri katika kipindi hiki cha usajili kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Septemba 6, mwaka huu, na tayari baadhi ya wachezaji wa timu zilizoshuka daraja wanasajiliwa na zilizobaki au kuendelea kuwapo kwenye ligi hiyo.

**Ikumbukwe kuwa msimu huu zimeshuka timu tano ambazo ni Mbao FC na Alliance FC zote kutoka Mwanza, Ndanda FC ya Mtwara, Lipuli ya Iringa na Singida United.**

Pamoja na timu hizo kuteremka daraja, huku zikisubiri kucheza Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, baadhi ya wachezaji wa timu hizo wamerudi kucheza Ligi Kuu kwa kusajiliwa na timu mbalimbali. Mwandishi wa makala haya amekusanya baadhi ya majina ya wachezaji ambao timu zao zimeshuka, lakini wamesajiliwa na zingine za Ligi Kuu.

**WAZIRI JUNIOR- YANGA**

Jina lake halisi ni Waziri Shentembo, ambaye msimu uliopita alifunga mabao 14 akiichezea Mbao FC. Kwa bahati mbaya hayakuisaidia timu hiyo kubaki Ligi Kuu.

Mbao imeshuka, lakini yeye hajashuka, badala yake amejiunga na Yanga, hivyo msimu unaofuata mashabiki wataendelea kumuona akiwa na timu tofauti kabisa.

**DAVID KAMETA- SIMBA**

Ni beki wa kulia ambaye amesajiliwa na Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara Simba akitokea Lipuli FC iliyoshuka daraja.

Kameta ambaye anajulikana kwa jina la Duchu, akiwa amefunga mabao matatu msimu uliomalizika, ni mmoja wa wachezaji ambao wamebaki Ligi Kuu licha ya klabu aliyokuwa akichezea kushuka.

**MARTIN KIGGI- KMC**

Msimu huu aliichezea Alliance FC na kumaliza ligi akiwa ma mabao saba. Straika huyu wa zamani wa Ndanda FC, msimu ujao ataonekana amevaa jezi ya KMC, akisajiliwa kwa mkataba wa mwaka mmoja baada ya timu yake ya Alliance kushuka daraja, lakini yeye bado yupo sana.

**DAVID MWASSA- KMC**

Ni beki wa kati aliyekuwa akiichezea Lipuli FC ambayo nayo mwisho wa msimu uliomalizika ilishuka daraja. Kwa sasa amesajiliwa na KMC kwa mkataba wa miaka miwili, hivyo wakati baadhi ya wachezaji wenzake wakisubiri Ligi Daraja la Kwanza, yeye anasubiri Ligi kuu akiwa na timu yake mpya.

**STEVEN SEY- NAMUNGO FC**

Straika huyu kutoka nchini Ghana, alimaliza ligi kwa kufunga mabao manne akiwa na Singida United ambayo imeshuka daraja. Kwa sasa amesajiliwa na Namungo FC kwa mkataba wa miaka miwili, hivyo amebaki Ligi Kuu, timu yake ikiporomoka.

**FRED TANGALO- NAMUNGO FC**

Klabu ya Namungo FC pia imemsajili kiungo Fred Tangalo kutoka Lipuli FC iliyoshuka daraja. Tangalo naye anakuwa ni mmoja wa wachezaji ambao wameshuka na timu zao, lakini wao wamerejea kwenye Ligi Kuu wakiwa na timu zingine.

**GEORGE WAWA- DODOMA JIJI**

Ni beki wa pembeni aliyekuwa akikipiga na Singida United ambayo imeshuka daraja. Yeye amebaki Ligi Kuu akiwa amesajiliwa na timu mpya iliyopanda daraja na itacheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu. Huyu si mwingine ni George Wawa.

**SEIF KARIHE- DODOMA JIJI**

Karihe ni straika wa zamani wa Azam, lakini msimu ulioisha alikuwa akiichezea Lipuli FC.

Baada ya timu hiyo kushuka daraja, bila kuchelewa amesajiliwa na Dodoma Jiji na msimu unaokuja ataonekana akivaa jezi za timu hiyo inayocheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza.

**ISRAEL PATRICK - KMC**

Huyu ni beki wa pembeni aliyejiunga na timu ya KMC akitokea Alliance FC. Anakuwa ni mmoja wa wachezaji walioiacha timu ishuke, lakini wenyewe wamerejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**TARO JOSEPH- MBEYA CITY**

Timu ya Mbeya City ambayo iliponea chupuchupu kushuka daraja kwenye mechi ya mchujo dhidi ya Geita Gold. Kwa kuimarisha kikosi chake, imemchukua Taro Donald Joseph kutoka Ndanda FC ambayo imeshuka daraja. Mchezaji huyo alikuwa kwenye kikosi hicho kilichoshuka, lakini sasa ameibukia Mbeya City iliyopo Ligi Kuu.

**SAMUEL MAURU- MBEYA CITY**

Ni mchezaji wa Ndanda ambaye baada ya kuteremka daraja, yeye akaondoka kwenye timu hiyo na kwenda kujiunga na kikosi cha Mbeya City kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**BABILAS CHITEMBE- MBEYA CITY**

Alishuka na timu ya Mbao FC, lakini sasa amesajiliwa na Mbeya City na kuendeleza usemi kuwa inashuka timu, lakini wachezaji hawashuki, wakiwa na uwezo wanabaki Ligi Kuu.

**GEORGE SANGIJA- MBEYA CITY**

Huyu ni mchezaji wa zamani wa Mbao FC, lakini msimu uliomalizika alikuwa akiichezea Singida United ambayo imeshuka. Ni mmoja wa wachezaji waliobaki Ligi Kuu baada ya timu zao kuteremka daraja.

**OMARI HAMISI- IHEFU FC**

Ni kiungo aliyekuwa akiichezea Ndanda FC na kufunga mabao matatu kwenye Ligi Kuu msimu uliomalizika. Baada ya timu yake kushuka daraja, yeye amejiunga na timu iliyopanda daraja ya Ihefu FC na ataonekana tena kwenye ligi.

**PAUL LUYUNGU- IHEFU FC**

Ni mchezaji aliyefunga mabao mawili akiwa na Lipuli iliyoshuka daraja. sasa ataonekana akiwa amevaa jezi ya Ihefu kwa msimu ujao wa ligi.

**JORDAN JOHN- IHEFU FC**

Moja ya wachezaji waliojitahidi sana kuibakisha Mbao FC kwenye Ligi Kuu, lakini ikashindikana. Alifunga jumla ya mabao sita. Ametangazwa kuwa ni mchezaji wa Ihefu FC. Ikumbukwe pia kuwa Ihefu ndiyo iliyoishusha Mbao FC kwenye mechi ya mchujo.

**JE, WAJUA?**



TANGU msimu wa 2009-10, ubingwa wa Ligi ya Europa umekuwa ukitwaliwa na kocha Mhispania, ikiwa ni mara sita katika fainali 11 (Unai Emery x3, Quique Sanchez Flores, Rafael Benitez, Julen Lopetegui-pichani).



# Kongamano kuombea uchaguzi kufanyika leo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KONGAMANO kubwa la kuombea amani kwenye Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu linatarajiwa kufanyika leo mkoani Dodoma na litahudhuriwa na waumini wa madhehebu yote nchini.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano ya Maadili na Haki za Binadamu Tanzania, Shekhe Mussa Salim, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa. Shekhe Mussa alisema kongamano hilo litawapa fursa viongozi wa dini kutoa mwongozo na mawaidha kwa wananchi kuelekea kwenye uchaguzi mkuu huo.

"Sisi wote ni wadau hivyo tuhakikishe uchaguzi huu unakwenda salama na kwa amani, uchaguzi utapita ila Tanzania itabaki, hivyo viongozi wataisihi NEC isimamie haki na Watanzania washiriki kwenye uchaguzi huo," alisema.

Alisema kila Mtanzania anapaswa kuona kuwa ni haki yake kushiriki kwenye uchaguzi huo kwa kuhakikisha anajitokeza kumchagua kiongozi ambaye anadhani anafaa kuongoza kwa miaka mitano.

Alisema jumuiya hiyo ilianzishwa mwaka 2016 kwa ajili ya kuwaelimisha Watanzania kuhusu umuhimu wa kudumisha amani na utulivu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa na mtu mmoja mmoja.

Alitaja dhumuni lingine ni kusaidia juhudi za serikali katika jitihada za kuondoa umaskini, ujinga na maradhi na kujenga mazingira ya kujitegemea miongoni mwa watu wake.

Shekhe Mussa alisema lengo lingine la jumuiya hiyo ni kukuza maelewano, ushirikiano na ujamaa miongoni mwa Watanzania bila kujali imani na itikadi za kisiasa.

Kadhalika, alisema lengo lingine kuwa ni kutafuta na kusimamia misaada inayopokewa kutoka kwa wafadhili mbalimbali na kuitumia katika miradi ya maendeleo kwa manufaa ya Watanzania.



Wakazi wa Mtaa wa Msangalale Dodoma Makulu jijini humo, wakifukia msingi uliochimbwa na Peter Jang'ombe kwenye eneo la nyumba wanayoishi Haghali Beleje (88) na dada yake Sonna Mudee (91) (hawapo pichani), baada ya eneo hilo kuwa na mgogoro kwa madai ya Halmashauri ya Jiji kummilikisha Jang'ombe bila utaratibu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vyakula, vipodozi vya mamilioni vyateketezwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Kati limeteketeza bidhaa za vyakula pamoja na vipodozi vilivyokwisha muda wa matumizi na vile vilivyo katazwa na serikali zaidi ya tani 2.2, vyenye thamani ya Sh. milioni 20.1

Akizungumza jana na waandishi wa habari, wakati wa uteketezaji wa bidhaa hizo katika dampo la Chidaya jijini Dodoma, Ofisa Mdhibiti Ubora wa Shirika hilo Kanda ya Kati, Sileja Lushibika, alisema zoezi hilo litakuwa endelevu na kuwataka wafanyabiashara kuacha kuuza bidhaa zilizoisha muda wake.

Alisema, bidhaa hizo ni kutoka katika mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora, ambazo zimeondolewa sokoni kutokana kumaliza muda wake na zingine zile ziliokatazwa na serikali, kwa kuwa na madhara kiafya.

Pia, alisema kuwa kati ya bidhaa hizo kilo 1,200 ni bidhaa za vyakula zilizokamatwa kutokana na kuisha muda wa matumizi sokoni zenye thamani ya Sh. milioni sita.

Aidha, alisema kuwa kilo 820, ni vipodozi vilivyomaliza muda wa matumizi ambavyo vilikutwa bado vipo sokoni vyenye thamani ya Sh. milioni 10.

"Lakini kilo 180, ni vipodozi ambavyo vimekamatwa na tunaviteketeza leo ambavyo hivi ni vile vilivyopigwa marufuku na serikali kutoka na kusababisha madhara mbalimbali ya kiafya kwa watumiaji wake ambavyo vinathamani ya Sh. milioni nne," alieleza Lushibika.

Kadhalika, Lushibika, aliwataka wafanyabiashara kuwa waaminifu kwa kuacha kuuza bidhaa zilizokwisha muda wake, kwani watakaobainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Wafanyabiashara wanatakiwa kuwa waaminifu kama wanaona kuna bidhaa imekwisha muda wake katika stoo zao, wawasiliane na sisi tuwaelekeze namna bora ya kuziteketeza na siyo kuendelea kuziacha katika soko," alisema.

Aliwataka watumiaji wa bidhaa mbalimbali nchini kuwa na utamaduni wa kusoma taarifa za muda wa matumizi kabla ya kuanza kuzitumia.

Vile vile, alisema TBS pekee yake haiwezi kukomesha tabia ya wafanyabiashara kuuza bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi bila jamii kushirikiana katika janga hilo.

Lushibika alieleza kuwa uwepo wa bidhaa zilizomaliza muda wa matumizi sokoni, kunaathiri afya za Watanzania ambao ndiyo mtaji mkubwa kufikia uchumi wa kati juu 2025.

Naye, Ofisa Usalama wa Chakula kutoka TBS, Vincent Tarimo, alisema kuwa watumiaji wa bidhaa mbalimbali wanatakiwa kuwa makini wanapoingia sokoni kujitafuta mahitaji.

"Wananchi pia tunatakiwa kuacha matumizi ya bidhaa za vipodozi zilizopigwa marufuku na serikali kwani zinachangia kwa kiasi kikubwa kuathiri afya zetu na kuipa mzigo mkubwa serikali," alisema Tarimo.

# Wahariri wafundwa kampeni za uchaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAHARIRI nchini wamewataka wagombea wa nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu 2020, kuacha kutumia lugha za matusi katika mikutano yao ya kampeni ili wapate nafasi katika vyombo vya habari.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika mkutano wa mwaka wa wahariri wa vyombo vya habari nchini, Mhariri kutoka Uhuru Media Group (UMG), Kiondo Mshana, alisema mgombea atakayetumia matusi hapaswi kupewa nafasi.

Alisema wagombea wote wanapaswa kueleza sera zao na namna watakavyowasaidia wananchi katika kujikwamua na kero mbalimbali na sio kutoa matusi katika mikutano yao ya kampeni.

"Vyombo vya habari vitatoa nafasi kwa wagombea wote na kwa wale ambao watajikita katika kutumia lugha za matusi katika uchaguzi mkuu 2020, basi wanatakiwa kunyimwa nafasi kwani kama chombo cha habari hatuwezi kutumika kufikisha matusi kwa jamii," alifafanua Mshana.

Pia, alisema siyo kweli kuwa vyombo vya habari nchini vimekuwa na ubaguzi katika kuwatumia baadhi ya wagombea na wengine kuwanyima nafasi.

"Siyo kweli sisi tunaangalia misingi ya habari lazima iwe na ukweli, lakini hatuwezi kutoa kitu ambacho mgombea anakitaka hata kama itakuwa ni matusi, hivyo basi habari yenye matusi haita pewa nafasi," alisema. Mhariri wa gazeti la Mtanzania Kulwa Kaledia, alisema wagombea wanatakiwa kueleza katika mikutano yao namna watakavyozishughulikia kero mbalimbali za wananchi wao katika mikutano hiyo na kuacha kutoa matusi.

"Wagombea wanatakiwa kueleza namna watakavyoshughulikia matatizo ya wananchi wao watakapopata nafasi za uongozi na siyo matusi kwa wengine," alifafanua Kaledia.

Jane Mihanji kutoka UMG, alisema wahariri wanapaswa kufuata taratibu na sheria za uchaguzi kwa mujibu wa sera za vyombo vyao.

Alisema kawaida vyombo vinapaswa kuwapa nafasi sawa wagombea wote bila kujali ukubwa wa chama, lakini vipo baadhi, ambavyo vipo kwa ajili ya kutetea propaganda za chama kingine.

"Kama mimi nipo katika chombo cha Uhuru, hivyo ni lazima kuwa mstari wa mbele katika kutetea Chama Cha Mapinduzi, ili kuzipigania kindakindaki propaganda za chama, lakini kwa vingine vinapaswa kutoa usawa kwa wagombea wote," alisema Mihanji.





## CCM yatamba kuzoa majimbo yote ya Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimejinadi kuwa kitashinda majimbo yote ya mkoa huo kwenye uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu kwa maelezo kuwa kimejiandaa vizuri kuliko vyama vingine.

Hayo yalisemwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya chama hicho kuelekea uchaguzi huo, ambapo alisema chama hicho kina sera ambazo zinakubalika.

Alisema kwa sasa chama hicho baada ya kuwateua watu watakaopeperusha bendera kwenye majimbo yote, kinaendelea na utaratibu wa kuwasimamia wagombea wake ili kuhakikisha wanajaza fomu kwa usahihi.

Alisema kwa kuzingatia sheria za uchaguzi, chama hicho kinasubiri mpaka Agosti 26, mwaka huu pazia la kampeni litakapofunguliwa ili kianze kutangaza sera zake kwa wananchi.

"Wagombea wetu wamechujwa kwa kuzingatia taratibu na kanuni za chama, tumewateua wale ambao wanakubalika, lakini chama chetu kimefanya mambo ambayo yanaonekana kwa watu na hayahitaji mtu awe na elimu kubwa ili ayaone na kuyaelewa," alisema Madodi.

Alisisitiza kuwa chama hicho hakina makundi kama baadhi ya watu wamekuwa wakikitafsiri, na kwamba kitaendelea makundi ya chama hicho huvunjwa baada ya kura za maoni na uteuzi wa wagombea kuteuliwa.

Alisema chama hicho pia kina utaratibu wa kuwatumia waliokuwa washindani wa wateule kwenye kunadi sera za chama ili kuhakikisha ushindi unapatikana kwa kishindo.

# Kituo usambazaji teknolojia, maarifa kilimo chaanzishwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imeanzisha kituo maalumu cha usambazaji wa teknolojia na maarifa ya kilimo bora kwa wananchi ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Kituo hicho kimeanzishwa katika viwanja vya Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) vya John Mwakangale jijini Mbeya na kitakuwa kinafanya kazi kwa mwaka mzima, ambapo vipando vya mazao mbalimbali vimeanza kuandaliwa.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kituo hicho, Mkurugenzi wa TARI- Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema elimu itakuwa inatolewa kwa nadharia na vitendo katika eneo hilo, na kwamba mashamba ambayo huwa yanatumika kwenye maonyesho ya Nanenane ndiyo yatatumika.

Alisema jengo la taasisi hiyo ambalo huwa linatumika wakati wa maonyesho ya Nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ndilo litakuwa linatumika kama darasa la kuwafundishia wananchi nadharia za kilimo kabla ya kuwapeleka shambani kujifunza kwa vitendo.

Dk. Bucheyeki alisema waliamua kuanzisha kituo hicho, ili kuwasaidia wananchi ambao huwa wanakosa nafasi ya kuhudhuria maonyesho ya Nanenane ambayo hufanyika kwa muda wa siku nane pekee.

"Kuna wataalamu wa kutosha ambao tumewahamishia hapa, watakuwa wanafanya kazi muda wote katika eneo hili, eneo hili lipo ndani ya taasisi yetu, kwa hiyo itakuwa rahisi wananchi kujifunza hapa na hata kule kituo kikuu," alisema Dk. Bucheyeki na kuongeza:

"Maonyesho ya Nanenane huwa yanafanyika kwa muda wa siku nane pekee, na kuna baadhi ya wananchi huwa wanakosa nafasi ya kuhudhuria maonyesho hayo, sasa hiki kituo ni cha kudumu mwaka mzima kitawasaidia."

Msimamizi wa kituo hicho, Lusungo Paul, alisema mpaka sasa kituo hicho kimeanza kupokea watu mbalimbali ambao wanaenda kujifunza wakiwamo wanafunzi wa vyuo mbalimbali vya kilimo.

Alisema walengwa wa kunufaika na kituo hicho ni wakulima mmoja mmoja, vikundi vya wakulima, mashirika ya umma na binafsi, mikoa na halmashauri za mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na wadau wengine wa kilimo.

Paul kutoka Idara ya Usambazaji wa Teknolojia na Uhusiano wa TARI, alisema kituo hicho kitakuwa kinatumika kama wakala wa kusambaza teknolojia zinazozalishwa na taasisi hiyo, na kwamba kipo jirani na kituo cha Mabazi cha Nanenane, hivyo ni rahisi wananchi kukifikia.

"Tunaziomba mamlaka za serikali za mitaa hasa wakurugenzi wa halmashauri na hata taasisi zisizokuwa za serikali ziwalete wananchi kuja kujifunza teknolojia hapa ili wazalishe kwa tija na kuinua uchumi," alisema Paul.

Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa TARI, Dk. Ndabhemeye Mlengera, alisema kuanzishwa kwa kituo hicho ni mkakati wa Wizara ya Kilimo wa kuhakikisha kunakuwa na mwendelezo wa mafunzo ya kilimo kwa wananchi. Alisema moja kati ya mambo ambayo wananchi watafundishwa ni matumizi ya mbegu za mazao yakiwamo mahindi kwa kuzingatia aina ya hali ya hewa ya eneo wanalolima ili wanapoenda madukani kuzinunua wawe wana uelewa wa kutosha.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki (kushoto), akiwaeleza wanafunzi wa Chuo cha Kilimo cha Uyole jijini Mbeya ambao wanapata mafunzo ya kilimo kwa vitendo katika kituo cha usambazaji wa teknolojia. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Chalamila awaonya wanafunzi watakaoharibu miundombinu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewataka wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mkoani humo kuepuka kufanya vitendo vya kuharibu miundombinu ya shule zao, ili kuepuka kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Chalamila alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, mabweni na maabara katika shule mbalimbali wilayani Mbarali, ambayo inatekelezwa kwa ushirikiano wa wananchi na serikali.

Alisema serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo, na kwamba kitendo cha wanafunzi kuiharibu kinasababisha hasara kubwa.

Alisema hivi karibuni aliwashughulikia wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kiwanja wilayani Chunya waliochoma mabweni kwa kuwacharaza bakora na kuwaamuru walipe faini, ambapo zaidi ya Sh. milioni 100 zilipatikana na zikatumika kujenga mabweni mapya.

"Sasa hivi ikitokea wanafunzi wengine wakafanya tukio kama hilo, hatutawachapa wala kuwatoza faini, badala yake tutawapeleka kusikojulikana na watarudi kujenga majengo hayo wakiwa wamevalia sare za magereza, kwa hiyo msijiingize huko," alisema Chalamila.

Vilevile, alisema katika Shule ya Sekondari ya kutwa ya Mbeya (Mbeya day) kumeripotiwa baadhi ya wanafunzi kuwa na tabia mbaya kiasi kwamba wanafikia hatua ya kuwakunja walimu wao wakitaka kupigana nao.

Alisema vitendo hivyo ni utovu wa nidhamu, na vinawafanya wanafunzi kutofanya vizuri kwenye masomo, hivyo aliwataka wanafunzi hao kuacha tabia hiyo kwa maelezo kuwa vitawagharimu.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema inatekelezwa kwa ushirikiano kati ya wananchi na Serikali Kuu ambapo alisema serikali imetoa fedha.

Alisema baadhi ya miradi hiyo inatekelezwa kupitia mfumo wa lipa kulingana na matokeo (EP4R), na kwamba miradi inayotekelezwa kwa mfumo huo ni ujenzi wa bweni la wasichana, matundu ya vyoo na vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Mengele.

Alisema lengo la miradi mingine ya ujenzi wa miundombinu hiyo inatekelezwa katika Shule za Sekondari Iwindi na Mwakaganga pamoja na Shule ya Msingi Isisi ambako vinajengwa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo.

"Wananchi wanachangia nguvu zao kwa kuleta mchanga, mawe na tofali, lakini serikali imetoa fedha ambazo zinatumika kununua vifaa vingine na vilevile wananchi wanashiriki kwenye ujenzi," alisema Mfune.

Baadhi ya wanafunzi waliishukuru serikali kwa kuwaboreshea miundombinu huku wakiiomba kuboreshewa mazingira mengine yaliyobakia ikiwamo upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada.

Zacharia Abdalah, wa kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Mengene, alisema maktaba ya shule hiyo haina vitabu vya kutosha na hivyo wanashindwa kujisomea.

Kadhalika, alisema shule hiyo haina mwalimu wa somo la Hisabati, hivyo wanalazimika kumtumia mwalimu anayetoka katika Shule ya Sekondari Rujewa, ambaye anakwenda mara moja moja shuleni hapo.



# IGP Sirro awataka viongozi wa dini kuhubiri amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Jeshi la Polisi Tanzania, IGP Simon Sirro, amesema jeshi lake halitopenda kutumia risasi wala mabomu katika uchaguzi.

Akizungumza na viongozi wa dini mjini hapa, alisema viongozi hao wana wajibu wa kuhubiri amani kabla na baada ya uchaguzi, ili wananchi waweze kupiga kura bila ya vikwazo vyovyote.

Alisema mtu yoyote atakayejaribu kuichafua amani iliyopo, jeshi lake litalazimika kutumia risasi na mabomu ili kupambana nao.

IGP Sirro alisisitiza kuwa ili amani iendelee kudumu nchini, viongozi wa dini wanajukumu la kuendelea kuhubiri amani kwa waumini wao ili iendelee kutawala nchini.

Aliwasisitiza wananchi kutojiingiza katika machafuko kipindi cha kuelekea uchaguzi na wakati wa uchaguzi na Jeshi la Polisi litamshughulikia kila atakayebainika kufanya vurugu kwa kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

"Viongozi wa dini mwendelee kulisaidia taifa hasa katika mahubiri yenu hasa kipindi hiki, na sisi jeshi tupo imara kuhakikisha amani inaendelea kutawala nchini," alisema.

Alisema kuwa uchaguzi usiwe chanzo cha kufanya vurugu na jeshi hilo lipo makini kulinda amani kipindi chote, hivyo wananchi wasijihusishe na makundi maovu.

Aliwataka kuendelea kutimiza wajibu wao kwa kufanya kazi yao kwa mujibu wa dini na kutokubali kutumiwa na wanasiasa kuchafua amani.

Naye Kamishna Ushirikishwaji wa Jamii Tanzania, Dk. Mussa Ali Mussa, alisema viongozi wa dini wana kila nafasi ya kushirikiana na viongozi wa Tume ya Uchaguzi kwa kuishauri ili nchi ibaki kuwa salama.

Alisema kuwa ni vyema viongozi wa dini wakaendelea kufuata miongozo ya viongozi wa dini waliotangulia kwa kufuata ukweli na maamrisho yao.

Aliwataka viongozi hao wa dini kutobaguana na kuendelea kuvumiliana hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

"Viongozi wa dini msipendelee sana kuhubiri siasa katika nyumba za ibada ili amani iendelee na mwendelee kukatazana maovu na mabaya ili nchi iweze kuwa na amani na ikivunjika haiwezi kurudi tena," alisema.

Kwa upande wao washiriki wa mkutano huo, waliahidi kuendelea kuhubiri amani ili taifa liendelee kubaki kuwa salama.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma (kushoto), akizungumza na wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na vyuo vikuu wakati wa semina maalum iliyofanyika katika ukumbi wa SUZA Mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mgombea uwakilishi apotea kitatanishi pwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ALIYEKUWA Kamishna wa Fedha wa Bajeti ya Serikali ya Zanzibar, Juma Juma (63), na mgombea kwenye kinyang'anyiro cha uwakilishi, Jimbo la Chaani, ametoweka katika mazingira ya kutatanisha.

Juma, mkazi wa Mbweni Mjini hapa ametoweka tangu Agosti 19, baada ya kutoka nyumbani kwake na kwenda kuogolea katika pwani ya Mazizini, mjini Unguja.

Akithibitisha kupotea kwa Juma, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Awadhi Juma, alisema familia yake iliripoti polisi kuwa baba yao hajarudi nyumbani na hajulikani alipo.

Alisema kwa maelezo ya familia yake, Juma huwa na tabia ya kwenda kuogolea nyakati za jioni na kisha kurejea nyumbani kwake, lakini kwa siku hiyo hakurudi.

Kamanda alisema Agosti 19, aliondoka nyumbani kwake akiwa na gari yenye namba za usajili Z 260 KN na kwenda kuogolea eneo la Mazizini, lakini hadi majira ya saa tatu usiku hakurudi nyumbani kwake jambo ambalo si kawaida yake.

"Familia ya Juma ilieleza kuwa ilipofika majira ya saa tatu usiku Agosti 19, mzazi wao hajarudi na kwenda katika ufukwe wa bahari ya Mazizini na kukuta gari yake ndani mkiwa na nguo zake, lakini mwenyewe hayupo," alisema Kamanda Awadhi.

Kadhalika, alisema haijafahamika kama Juma amezama baharini na kwamba Jeshi la Polisi linaendelea kufanya uchunguzi.

Juma pia ameingia katika kinyang'anyiro cha kugombea uwakilishi Jimbo la Chaani, Mkoa wa Kaskazini Unguja kupitia Chama Cha Mapinduzi na anasubiri jina moja litakaloteuliwa na Kamati Kuu ya CCM kuwa mgombea wa jimbo hilo.

# Wahitimu wapewa somo kujiunga elimu ya juu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewaomba wanafunzi wanaotarajia kujiunga na elimu ya juu kuchagua fani zilizowekewa vipaumbele na serikali.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya wahitimu wa kidato cha sita na stashahada, mjini hapa.

Alisema kama wanafunzi watachagua fani zenye upungufu wa wataalamu wataisaidia serikali yao kumaliza tatizo la uchache wa fani hiyo wazalendo na kumaliza tatizo la kutegemea kutoka nje ya nchi.

Waziri Pembe alisema kufanya hivyo pia kutasaidia kuepuka kukaa nje muda mrefu baada ya kumaliza masomo na kuingia kwenye ajira moja kwa moja.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inajivunia wataalamu wazalendo wa fani mbalimbali kwa kuongeza fursa za udhamini wa masomo kwa wanafunzi wanaofanya vizuri. Alisema wanafunzi wengi hawazingatii umuhimu wa fani hizo za vipaumbele ikiwamo taaluma za ualimu wa sayansi, fani za udaktari, mafuta na gesi na badala yake kusoma kwa kufuata mkumbo hali inayochangia kudumaza maendeleo ya nchi.

"Nchi yetu ina upungufu hasa wataalamu wa mafuta na gesi na fani nyengine hivyo ni vyema kwa nyinyi wanafunzi kusoma fani hizi ili kusaidia kuziba mapengo yaliyokuwapo katika serikali yetu," alisema.

Aliwataka wanafunzi watakaobahatika kupata fursa za masomo hasa nje ya nchi kujiheshimu kwa kulinda mila, silka na utamaduni wa kizanzibari ili kuendelea kuipa heshima nchi yao.

"Chonde chonde mkipata fursa hii basi ipeni heshima Zanzibar, nendeni kwa lengo moja la kutafuta elimu na sio kufanya mambo ambayo hayana mustakabali mwema wa maisha yenu na nchi yenu," aliwaasa wanafunzi hao.

Aliwataka wanafunzi hao kuzitumia bodi zote za mikopo ikiwamo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuomba mikopo na watakaobahatika kupata bodi zote zitoe taarifa.

Aliyaomba mashirika ya kifedha kutengeneza mazingira ya kuwasaidia wanafunzi wanaofanya vizuri ili waweze kupata fursa ya kusoma na kuisaidia serikali kuendelea kuinua sekta ya elimu ili taifa liendelee kupiga hatua kiuchumi.

Aliwapongeza wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani yao ya taifa ya kidato cha sita hasa wanawake na kuwasisitiza kusoma kwa bidii.

Naye Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu Zanzibar, Iddi Haji Khamis, alisema lengo la mafunzo hayo ni kutekeleza agizo la Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed, la kutaka kuwapatia elimu wanafunzi kujua taratibu mbalimbali kabla ya kuingia vyuoni. Alisema utaratibu huo unasaidia kujenga uelewa na hamasa kwa wanafunzi ya mifumo bora ya kuomba vyuo na kufanya maamuzi sahihi ya kuendelea na masomo nje na ndani ya nchi.

Mwakilishi kutoka Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Francis Mshumba, alisema serikali zote mbili zimeongeza bajeti ya mikopo kwa lengo la kuhakikisha vijana wa kitanzania wanapata fursa ya kusoma.

Aliwasisitiza vijana kutumia fursa hizo kwa vyuo vilivyothibitishwa na serikali nchini, ili kunusuru gharama nyingi zinazotumika kwa vyuo vya nje.

Katika mafunzo hayo mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwamo huduma za bodi za mikopo ya Zanzibar na Tanzania Bara, fani muhimu za gesi na mafuta, kuomba kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA, Nyumba ya Gorofa 1, inauzwa na fremu za biashara, umeme na maji. Inafaa kwa kuishi na kwa biashara. Mawasiliano: 0757 079057.**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



115867002

**Happy Mwansana Sanga** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Kilichotolewa kwa mtahiniwa namba **S0653/0019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2015 katika shule ya sekondari Mwakavuta wilayani Makete yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Taarifa ya polisi : **RB NO; NJO/MAK/RB/561637/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ESTHER SOLOMON HANGA**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **Toyota Alphard**
Yenye namba ya usajili **T986 DMA** Iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
Chasis no **ANH100024903,** Engine no **2NZ0031886.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**DOD/DOD/RB/582241/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA (W) TARIME**
**MAOMBI NA. 40 YA 2020**
**ALBETUS OTIENO SAUSI..................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**

1. **SARONGE MATOYO**
2. **ANNA SARONGE MATOYO .............WAJIBU MAOMBI**

**MJIBU MAOMBI SARONGE MATOYO POPOTE ULIPO.**

Fahamu kwamba mleta maombi ALBETUS OTIENO SAUSI ameleta maombi Na. 40/2020, dhidi yako.

Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi hayo unatakiwa ulete majibu yako na uwepo barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, tarehe 11/09/2020, siku ambayo maombi yamepangwa kutajwa.

Endapo hutatekeleza hayo, shauri litaendelea upande mmoja dhidi yako na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 12/08/2020.

NGUKULIKE, N.O
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TARIME.

115868402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FARAJA ELIAS SAMHENDA**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **NISSAN EXTRAIL** yenye namba za usajili **T571 CUM** Chassis no. **NT30128772,** Engine no. **QR20482695A.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/KIJ/RB/609702/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MUSSA MOHAMED MTORE**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **Toyota Kluger**
Yenye namba ya usajili **T871 DFS**
Iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**MWA/NY/RB/599955/2020**

115867102


*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza*

*Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Jamii ya Wamasai yajenga shule kuunga mkono serikali

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

KATIKA kuhakikisha sekta ya elimu inakua nchini, jamii ya wafugaji wa kabila la Wamasai imeamua kuunga mkono juhudi za serikali kwa kujenga vyumba vitatu vya madarasa ya shule ya msingi kwa ajili ya watoto wao kupata elimu.

Kiongozi wa kimila wa kabila hilo, Olewaso Timoyo, alisema wameamua kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kwa kujenga vyumba vitatu vya madarasa ili kukuza sekta ya elimu nchini.

"Watoto wengi hawajui kusoma wala kuandika na hii inatokana na wao kuwa ndiyo wachungaji wa mifugo yetu, hivyo awali hatukuona sababu ya kuwapeleka shule, lakini kwa sasa tumeona umuhimu wa elimu hapa nchini," alisema Timoyo.

Alisema kuwa baada ya jamii hiyo kutambua umuhimu wa shule kwa watoto wao, wafugaji wote wa kabila hilo wameamua kujenga shule kwa kutumia mali na nguvu zao na kila mtoto wa Kimasai ni lazima atakwenda shule.

Alisema baada ya ujenzi wa vyumba hivyo kukamilika utawekwa utaratibu wa kuhamasishana kila mtoto aende shule kwa kuwa azma ya jamii hiyo ni kutokomeza mila na desturi zinazowaangamiza watoto hususani wa kike.

Kiongozi huyo wa kimila alisema mbali na kuwa kijiji hicho cha Kisaki kuwa na shule ya msingi, watoto wa kifugaji hawakuwa na mwamko wa kwenda shule na baada ya madarasa hayo kukamilika ni lazima watasoma. Aliipongeza serikali kwa jitihada za kuboresha sekta ya elimu nchini na kuwa jamii hiyo itakuwa mstari wa mbele kukuza elimu kijijini hapo ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto mbalimbali shuleni.

"Tumeamua kuunga mkono juhudi za serikali yetu, hivyo sisi wafugaji wa kijiji hiki cha Kisaki tutakuwa mstari wa mbele kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika shule yetu hii, lakini siku za usoni tutajenga sekondari," alisema Timoyo.

Mkazi wa kijiji hicho, Saitoti Mwalimu, alisema asilimia kubwa ya watoto wa kifugaji wa kabila hilo hawajui kusoma wala kuandika kutokana na wazazi wao kutokuwa na mwamko wa elimu na kwamba sasa wataelimika kutokana ushawishi mkubwa uliopo.

Mwanakijiji huyo alisema kuwa wafugaji hao wametambua umuhimu wa kuwapeleka watoto wao shule, ili wakaelimike ndiyo maana wameamua kuuza baadhi ya mifugo yao wajenge madarasa ya watoto wao kusoma.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, amepongeza kitendo hicho na kuahidi kutoa shilingi milioni tatu kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba hivyo na ukarabati wa shule.

# RC aipa kampuni siku 7 kulipa wafanyakazi mil. 100/-

**Na Francis Godwin,** IRINGA

SERIKALI mkoani Iringa imetoa wiki moja kwa kampuni ya Mufindi Tea Company (MTC), kuwalipa mshahara Sh. milioni 100 wafanyakazi wa kampuni hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alitoa agizo hilo jana katika kijiji cha Sawala, Wilaya ya Mufindi baada ya wafanyakazi wanaodai mishahara yao kwenda na mabango ya malalamiko kwenye mkutano wake wa kukagua miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

Kufuatia malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa alilazimika kumpigia simu Meneja wa kampuni ya MTC na kumpa maelekezo ya kuwalipa mishahara wafanyakazi hao ndani ya wiki moja pamoja na kufika katika kijiji cha Sawala kufanya mkutano wa hadhara na wafanyakazi hao ili kuondoa tofauti zao.

Pia, aliagiza kampuni hiyo kuanza kuwalipa wakulima wa chai Sh. milioni 300 wanazodai. Hapi alisema kampuni hiyo mbali ya kushindwa kuwalipa mishahara wafanyakazi na wakulima wanaodai pesa zao, imeshindwa kupeleka michango ya wafanyakazi NSSF jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa sheria ya kazi, hivyo kumtaka mwajiri wa kampuni hiyo kutekeleza wajibu huo.

Aliagiza NSSF kumbana mwajiri kupeleka michango ya wafanyakazi na kuhakikisha wanatekeleza taratibu za kuwapa adhabu ya faini ya asilimia tano kila mwezi ya michango waliyoshindwa kupeleka.

Awali, wafanyakazi hao walimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa kampuni hiyo imekuwa ikiwanyanyasa kwa kuchelewesha mishahara yao na kuua chama chao cha ushirika wa kuweka na kukopa SACCOS na uongozi wa mkoa kuingilia kati suala hilo.



Mkurugenzi Mkuu wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema (kulia), akizungumza na Baraza la Uongozi wa Chuo cha Usafirishaji (NIT), lilipotembelea Bandari ya Dar es Salaam wiki iliyopita. **NA MPIGAPICHA WETU**

# TPA, NIT kushirikiana kwa mafunzo

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA) imepanga kusaini makubaliano ya mkataba na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), ili kuwawezesha wafanyakazi wa bandari kupata mafunzo chuoni hapo.

Akizungumza baada ya Baraza la Uongozi wa chuo hicho kufanya ziara ya kikazi kulitembelea mamlaka hiyo, Mkuu wa Chuo cha NIT Prof. Zacharia Mganilwa, alisema katika mafunzo hayo, chuo kilishirikisha TPA na kuingiza mawazo yao katika mitaala mipya.

Alisema kabla ya kuanza kuitengeneza mitaala hiyo mipya ambayo imeishakamilika waliwashirikisha TPA ili wakianza kutoa kozi ziendane na mahitaji ya mamlaka hiyo na kuongeza rasilimali watu (wataalamu).

"Lengo kubwa la kuja hapa ni kuwaeleza kwamba mawazo yenu yote mliyoyatoa tumeyaingiza kwenye mitaala yetu mipya ambayo imeishakamilika na kuanzia Novemba tutaanza kudahili wanafunzi wapya wanaohusiana na upanuzi wa bandari," alisema Prof. Mganilwa.

Alisema kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Bandari hiyo, asilimia 50 ya wafanyakazi wa TPA ni wanafunzi kutoka NIT hivyo kutokana na mradi huo wa upanuzi wa bandari, mahitaji yao yataongezeka zaidi ndio maana katika ziara hiyo Baraza la Uongozi la Chuo limeshiriki ili wajue wanafunzi baada ya kumaliza wanakwenda wapi na pia wajue mahitaji muhimu ya wadau kama TPA ambao wanachangamoto.

Prof. Mganilwa aliongeza: Lazima changamoto za TPA wazichukue wazibadilishe ziwe fursa, mfano, upanuzi wa bandari uendane na malengo ya serikali hasa katika uchumi wa viwanda ambapo malighafi nyingi zitaagizwa kwa usafiri wa njia ya maji na pia kusafirisha malighafi nyingi zaidi kuliko vilivyo hivi sasa kwa hiyo kutahitajika wataalamu wa kuendana na kasi ya uchumi wa viwanda.

Mkurugenzi Mkuu wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema, alisema ujio wa Bodi ya NIT bandarini hapo unatarajiwa kufanikisha uboreshaji wa bandari kwa kujua namna ya kuanza kutoa mafunzo kwa wafanyakazi katika maeneo ya kuendesha mitambo na kuitengeneza, maeneo ambayo yanamahitaji makubwa kila siku.

Tunatarajia tutafanya nao kazi kwa kiasi kikubwa na nadhani ipo haja ya kuingia mkataba wa makubaliano ili kuangalia ni jinsi gani tutakuwa tunawapa mafunzo wafanyakazi wa mamlaka ya Bandari kwa kutumia NIT, ili kuongeza ufanisi wa bandari na kuendana na kazi ya upanuzi wa kina cha bahari ambao unaendelea kufanyika," alisema Lema.

Naye rais wa serikali ya wanafunzi NIT, Abel Joseph alisema, amefurahi kusikia kuwa watu ama nguvu kazi inayotoka NIT inakidhi matakwa na inafanya kazi kubwa kuhakikisha kuwa TPA inazidi kukua.





# CONTE AKINGIWA KIFUA INTER MILAN

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte na Inter Milan wanaonekana kuangalia uwezekano wa kuachana, lakini Rais wa zamani wa Nerazzurri hao, Ernesto Pellegrini, ambaye aliwaongoza kwa muda mrefu zaidi hataki jambo hilo litokee kwa sasa.

Kipigo cha mabao 3-2 kweye fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla Ijumaa, maana yake ni kwamba, Conte amemaliza msimu wake wa kwanza na Inter bila taji lolote.

Na kocha huyo wa zamani wa Juventus na Italia, mwenyewe alishakuwa na shaka juu ya majaliwa yake baada ya kunukuliwa akisema Inter lazima ianza mipango mipya na “mimi au bila mimi”.


Pellegrini, ambaye alikuwa rais wa Inter kutoka mwaka 1984 hadi 1995, ameonyesha kwamba Conte anatakiwa kuhamasishwa kuingia msimu wa pili kuliko kuondoka sasa.

Inter ilimaliza nafasi ya pili kwenye Serie A, na kufika nusu fainali ya Coppa Italia na kutinga fainali ya Europa ikiwa ni mafanikio makubwa kwa kipindi cha miaka 10.

“Natumaini kwamba kila kitu kitapata suhuhilo. Kama anataka kuondoka, litakuwa jambo jingine, lakini matumaini yangu atabaki,” alisema Pellegrini akiiambia Radio Sportiva.

“Bila shaka ni swali la kumuuliza Conte na kujua nini kilichopo kwenye akili yake, sababu ya kubwatuka kwake hata siielewi.

“Mashabiki wana furaha na matokeo. Bila shaka kama tungeshinda lingekuwa jambo bora zaidi.”



# Ljungberg aachana rasmi na Arsenal

**LONDON,** England

FREDDIE Ljungberg ameondoka katika nafasi yake ya kocha msaidizi katika klabu ya Arsenal ili kutafuta nafasi zaidi ya ukocha.

Ljungberg aliteuliwa kocha msaidizi wa klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England baada ya kufukuzwa kwa Unai Emery Novemba mwaka 2019.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Sweden, ambaye alikuwa sehemu ya kikosi cha Arsene Wenger kilichomaliza msimu wa 2003-04 bila kupoteza mchezo, alibakia kwenye benchi la ukocha wa Arsenal baada ya kuteuliwa kwa Mikel Arteta.

Ljungberg, ambaye aliziongoza timu za klabu hiyo za umri wa chini ya miaka 15 na 23, sasa ameamua kuondoka na kuangalia hatua inayofuata.

Mkongwe huyo mwenye umri wa miaka 43, alisema: “Nimeamua kuondoka kwenye nafasi yangu ya kocha msaidizi wa kikosi cha kwanza hapa Arsenal ili kwenda kupata uzoefu mwingine.

“Nimekuwa na klabu hii tangu mwaka 1998 na nashukuru kwa nafasi waliyonipa nikiwa mchezaji na kocha.

“Namtakia Mikel na timu yote mafanikio katika msimu unaokuja. Nawashukuru pia mashabiki kwa sapoti yao.”

# Messi haondoki Barca-Ronaldo

**LISBON,** Ureno

LIONEL Messi ni “vigumu sana” kuondoka Barcelona kabla ya msimu wa 2020-21, kwa mujibu wa gwiji wa Brazil, Ronaldo.

Mabadiliko ya kukisafisha kikosi yameanza pale Barca baada ya kunyanyaswa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mikononi mwa Bayern Munich, huku Kocha Mkuu, Quique Setien na Mkurugenzi wa Michezo, Eric Abidal nafasi zao zikichukuliwa na Ronald Koeman na Ramon Planes.

Uchaguzi wa urais pia umesogezwa mbele hadi Machi. Kwa mujibu wa ripoti, wachezaji wengi wa kikosi cha kwanza wakiwamo Jordi Alba na Sergio Busquets, wamewekwa sokoni baada ya kipigo cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern, huku kukiwa na matarajio tofauti kwa Messi.

Hata hivyo, mshindi huyo mara sita wa Ballon d’Or amedaiwa kumjulisha Koeman kwamba hayaoni majaliwa yake hapo Camp Nou.

Messi yupo kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake na Barca, lakini straika wa zamani wa klabu hiyo, Ronaldo, ambaye anaimiliki klabu ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Real Valladolid, anaamini athari ya matatizo ya kifedha yaliyotokana na mlipuko wa virusi vya corona yatasababisha usajili kuwa mgumu.

“Ni vigumu sana kwa Messi kuondoka Barcelona, hasa kutokana na tatizo la kifedha lililoikumba Ulaya,” alisema Ronaldo.

“Messi ndiye alama ya timu na kama ningekuwa Barcelona singeweza kumuachia aondoke kwa namna yoyote.

“Messi hayupo kwenye mahusiano mazuri na Barcelona, sidhani kama ataacha mapenzi yake kwa timu.

“Amechukia kwa sababu ya kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

“Messi anawahitaji wachezaji wenzake kumsajili, kama wanavyofanya, na Barcelona watatakiwa kufikiria kitu fulani tofauti kwa ajili ya msimu ujao. Kumuachia mchezaji muhimu kuondoka si suluhisho.”



# Barcelona yawania kumsajili Angelino

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeonyesha nia ya kumtaka mlinzi wa pembeni wa Manchester City, Angelino, huku klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England ikitaja bei yake kuwa ni euro milioni 30.

Angelino alijiunga tena na City kutoka PSV mwaka jana, lakini alishindwa kuthibitisha kiwango chake chini ya kocha, Pep Guardiola.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, amecheza mechi 12 tu katika mashindano yote, akianza kwenye mchezo wa kipigo dhidi ya Liverpool na Manchester United kabla ya kusajiliwa kwa mkopo kule RB Leipzig, Januari.

Alionyesha kiwango cha kuvutia katika kikosi hicho cha kocha, Julian Nagelsmann na alitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kiwango hicho kimewavutia Barcelona iliyopo chini ya kocha mpya, Ronald Koeman.

Stats Perform News inaelewa kwamba, City wameshapanga bei ya Angelino, ambayo inatajwa kuwa euro milioni 30.

Hata hivyo, Leipzig ilikuwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja Angelino.







# MARTIAL AKIRI SOLSKJAER KUMUINUA KIWANGO

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Anthony Martial, amesema kuaminiwa na kocha Ole Gunnar Solskjaer na kuongezeka kwa mechi za kucheza ndiyo sababu ya kuwa na msimu wa kuvutia kwake wa 2019-20.

Martial alimaliza msimu huo kama kinara wa mabao wa United akitikisa nyavu mara 23 katika mashindano yote, moja zaidi ya mchezaji mwenzake, Marcus Rashford.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24, alifunga mabao 17 kwenye Ligi Kuu kuisaidia United kumaliza nafasi ya tatu na kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku akifunga manne wakati klabu hiyo ikiishia nusu fainali ya Kombe la Europa.

Ulikuwa msimu bora zaidi wa mabao kwa Martial na United tangu alipowasili akitokea kwa miamba wa Ligue 1, Monaco mwaka 2015 na ameelezea sababu ya kuwa na kiwango bora hapo Old Trafford.

"Nafikiri sasa ni ukweli kwamba nimefurahia zaidi mechi nyingi za kucheza. Nimecheza katika kila mchezo na nafikiri ni kuhusu kiwango changu," alisema Martial, ambaye hakuwa kwenye kiwango kizuri chini ya kocha wa zamani, Jose Mourinho, akiliambia jarida la Inside United.

"Katika misimu niliyopita, sikuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara; muda mwingi nilikuwa benchi na mara chache nilianza, kitu ambacho kilikuwa kigumu kwangu."

# *Klopp: Tupo tayari kuivaa Arsenal*

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesisitiza Liverpool lazima ifungue silaha zote kwenye mchezo wa wikendi ijayo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Arsenal.

Mshindi huyo wa Kombe la Ligi Kuu ya England yupo na kikosi hicho nchini Austria kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa ligi, wakiwa na mechi za kirafiki dhidi ya Stuttgart na Salzburg kabla ya kusafiri kwenda kwenye dimba la Wembley.

Alisema kwamba timu yake iko tayari kwa ajili ya msimu mpya, lakini jambo la kwanza ni mchezo wao wa Ngao ya Jamii dhidi ya Arsenal.

"Kuelekea mchezo huu, tunajaribu kwa hali na mali kuwa tayari kwa ajili ya Arsenal, lakini hata baada ya hapo kuna wiki nyingine mbili."

Kikosi hicho cha Klopp kitawavaa Arsenal ambao ni mabingwa wa Ligi wa Kombe la FA Agosti 29, mwaka huu katika dimba la Wembley. Liverpool wataanza kutetea taji la Ligi Kuu dhidi ya Leeds United katika dimba la Anfield Septemba 12, mwaka huu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO KWA MBAPPE, AMKATAA NEYMAR REAL

●●● Ni uwekezaji, litakuwa jambo la maana zaidi kumsajili mchezaji kijana kati yao hao...

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

GWIJI wa Real Madrid, Luis Nazario de Lima maarufu zaidi kama Ronaldo, anaamini kwamba mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, wanatakiwa kumsajili, Kylian Mbappe badala ya mchezaji mwenzake wa Paris Saint-Germain, Neymar.

**Mbappe amekuwa akitajwa kuwaniwa na Madrid kwa muda mrefu, huku Los Blancos hao wakiripotiwa kumfikiria kwa usajili wa mwaka 2021.**

Nyota wa zamani wa Barcelona, Neymar - ambaye alijiunga na PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222 mwaka 2017, pia awali alikuwa akihusishwa na Madrid.

Lakini gwiji wa Brazil, Ronaldo na mshindi wa taji la LaLiga akiwa na Madrid msimu wa 2002-03, anaona nyota wa Ufaransa, Mbappe ndiye anayepaswa kusajiliwa Madrid badala ya raia mwenzake, Neymar na hii ni kutokana na umri.

"Kwa sasa, si sula la nani ni bora kuliko mwenzake, lakini Real Madrid kama inataka kufanya uwekezaji mkubwa, wanatakiwa kufanya kitu fulani kuhusu majaliwa yao ya baadaye," alisema Ronaldo akinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

"Neymar ana umri wa miaka 28 na Mbappe ana miaka 22.

"Ni uwekezaji, litakuwa jambo la maana zaidi kumsajili mchezaji kijana kati yao hao wawili."

Mbappe na Neymar jana Jumapili walikuwa uwanjani kuiwakilisha PSG dhidi ya Bayern Munich kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mjini Lisbon.

Miamba hao wa Ufaransa walicheza fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza katika historia yao.

Neymar - ambaye tayari alishinda taji la Ligi ya Mabingwa mwaka 2015 akiwa na Barca, ameshabeba mataji ya Ligue 1, Coupe de France, Coupe de la Ligue na Trophee des Champions msimu wa 2019-20.

## ZISIKUPITE

### BARCELONA KUMJIBU MESSI

BARCELONA inajiandaa kumjibu mshambuliaji na nahodha wao, Lionel Messi raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 34, kuhusu suala la kutaka kuondoka lililopo mikononi mwake. ***(Clarin, via Mirror Online)***

### ARSENAL PAZURI KWA GABRIEL

KLABU ya Arsenal inazidi kuongeza imani ya kumsajili mlinzi wa kati wa Lille na Brazil, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 22, lakini Manchester United imemwomba mchezaji huyo kuchelewa kutoa maamuzi. ***(Independent)***

### UNITED KUACHANA NA SANCHO

MANCHESTER United inaweza kuachana na mazungumzo ya makubaliano ya kumsajili winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, na watarudi tena mwakani. ***(Sunday Express)***

### WAMTAKA TAGLIAFICO

LEICESTER City inamwania mlinzi wa kushoto wa Ajax na Argentina, Nicolas Tagliafico mwenye umri wa miaka 27, kama mrithi wa Ben Chilwell, 23, anayewaniwa na Chelsea. ***(Mail on Sunday)***

### KIMYA KWA HAVERTZ

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayer Leverkusen, Rudi Voller amesema klabu hayo imetulia kuhusu hali ya kiungo wao, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21, wakati akiwa anahusishwa na Chelsea. ***(Star Sunday)***

### WOLVES KUMUUZA TRAORE

KLABU ya Wolves ipo tayari kumuuza winga wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 24, baada ya kocha, Nuno Espirito Santo kuambiwa atafute fedha zake mwenyewe kwa ajili ya usajili. ***(Sunday Mirror)***

### ARSENAL, BARCA KWA SARRARE

ARSENAL na Barcelona zinawania kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Malang Sarrare mwenye umri wa miaka 21, ambaye ni mchezaji huru kwa sasa pale Nice. ***(Mail Online)***

### BROOKS NJIA NYEUPE UNITED

MATUMAINI ya Manchester United kumsajili kiungo wa Wales, David Brooks mwenye umri wa miaka 23, yameimarika baada ya Bournemouth kubainisha kwamba hawatamzuia mchezaji anayetaka kuondoka. ***(Sun on Sunday)***

### ALCANTARA AWINDWA ARSENAL

ARSENAL imemuulizia kiungo wa Bayern Munich, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 29, lakini itahitajika kwanza mabingwa hao wa Ujerumani kupunguza bei yake. ***(Mail on Sunday)***

### VILLA YAMSAKA EDOUARD

KLABU ya Aston Villa imejipanga kutoa ofa ya pauni milioni 30 kwa ajili ya kumsajili straika wa Celtic na mchezaji wa timu ya Taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 21, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 22. ***(Sun on Sunday)***

### OCAMPOS KUMRITHI TRAORE

WOLVES inamwania winga wa Sevilla na Argentina, Lucas Ocampos mwenye umri wa miaka 26, kama mrithi wa Adama Traore. ***(Sky Sports)***

# HABARI MICHEZO

## Kichuya arejea Mtibwa Sugar

**Na Saada Akida**

WINGA wa Mabingwa wa Kandanda Tanzania, Simba, Shiza Kichuya, ameitosa Namungo FC na kuamua kujiunga na kikosi cha 'Wakata Miwa Manungu, Mtibwa Sugar kwa msimu mpya wa 2020/21.



Taarifa za uhakika zilizoifikia gazeti hili kutoka ndani ya Simba, zinaeleza Kichuya alitakiwa na Namungo na uongozi uliridhia, lakini chaguo lake limekuwa kwa timu yake hiyo ya zamani, Mtibwa Sugar.

"Simba iliridhia kumpeleka kwa mkopo Namungo kwa sababu kupata nafasi hapa itakuwa vigumu, hivyo kwenda huko atacheza ligi na mechi za kimataifa, lakini yeye amekataa na kuichagua Mtibwa Sugar," alisema mtoa habari wetu.

Alisema uongozi wa Simba umeheshimu maamuzi ya Kichuya na hivyo kumpa nafasi ya kuchagua timu ambayo anahitaji kuichezea.

Kocha Mkuu wa Mtibwa, Zubery Katwila alipotafutwa kuzungumzia juu ya nyota huyo, alisema kulikuwa na mapendekezo hayo na uongozi upo katika mazungumzo na Kichuya.

"Bado hajasaini, ila wapo katika mazungumzo naye, hivyo sijajua wamefikia hatua gani, pamoja na beki wa Nkana FC, Hassan Kessy," alisema Katwila .

## TBS wageukia Viwango Sports

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) wametakiwa kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara ili kujenga miili yao kiafya.

Rai hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa TBS, David Ndibalema, wakati wa ufunguzi rasmi wa Viwango Sports Bonanza lililohusisha wafanyakazi wa shirika hilo.

Ndibalema alisema unapokuwa na wafanyakazi wenye afya nzuri unakuwa na rasilimali ya watu wenye nguvu ambao wanafanya kazi vizuri na kwa ushirikiano.

Alisema Viwango Sports Bonanza ni la kwanza kufanyika katika shirika hilo na wanatarajia kuendeleza mashindano hayo kila mwaka kwa lengo la kuwakutanisha pamoja, wafanyakazi hao na kuwasaidia kuwa na utamaduni wa kuwakumbusha ufanyaji wa mazoezi.

"Hii ni mara ya kwanza kwetu kufanya Bonanza. Tumeona ni jambo zuri ambalo linawakutanisha wafanyakazi wetu wa idara zote na kuwajengea uwezo wa kujuana na kudumisha mahusiano yao ya kufanya kazi kwa ushirikiano zaidi," alisema Ndimalema.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Viwango Sport Bonanza, Lucas Gwila, alisema michezo inayochezwa ni pamoja na mpira wa miguu, kikapu, kuvuta kamba, michezo ya jadi, karata na kwamba walianza na mazoezi ya viungo kabla ya michezo hiyo.

# SARPONG AWATULIZA MASHABIKI YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA mpya wa Yanga, Mghana Michael Sarpong ameshusha mzuka wa mashabiki wa klabu hiyo, baada ya kuelezea furaha yake ya kujiunga na kuipigania.

**Mashabiki wa Yanga walikuwa na shauku kubwa ya kuona klabu hiyo ikisajili mshambuliaji kutokana na msimu uliopita safu ya ushambuliaji iliyokuwa ikiongozwa na David Molinga kushindwa kuwapa furaha waliyokuwa wakiitaka.**

Sarpong ambaye amejiunga na Yanga akitokea Rayon Sports ya Rwanda, anakuwa mchezaji wa tatu wa kimataifa kusajiliwa na klabu hiyo msimu huu baada ya viungo wawili raia wa DR Congo, Tusila Kisinda na Mukoko Tunombe waliotua wakitokea AS Vita ya kwao.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia Yanga, alisema lengo lake ni kuhakikisha anaisaidia klabu hiyo kufikia malengo yake.

Sarpong mwenye umri wa miaka 24, tayari ameungana na wenzake katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea viwanja vya Chuo cha Sheria jijini Dar es Salaam.

"Ninajisikia furaha kuwa mwanafamilia wa Yanga ninatambua hii ni timu kubwa na ina wachezaji wengi wazuri, hivyo nitashirikiana nao kutimiza malengo," alisema.

Mashabiki wa Yanga watakuwa na nafasi ya kuanza kuona ubora wa Sarpong wakati akitambulishwa Agosti 30, mwaka huu, kwenye kilele cha Wiki ya Wananchi katika Uwanja wa Mkapa.

Baada ya hapo wanaweza kuushuhudia zaidi ubora wake kwenye mechi za Ligi Kuu Bara watakapoanza na Tanzania Prisons Septemba 6, mwaka huu katika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam.

## KI-GOFU ZAIDI...



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, akicheza gofu wakati wa mashindano ya ndani ya mwezi yaliyoandaliwa na kampuni ya simu za mkononi ya Zantel na kufanyika katika viwanja vya TPDF Lugalo Golf jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *KVZ kuiwakilisha Z'bar Shirikisho Afrika*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KVZ imetwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, baada ya kuichapa Tekeleza kutokea Kisiwani Pemba kwa mabao mabao 3-1 katika mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa Gombani, Pemba.

Kwa ubingwa huo, KVZ sasa imekata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Katika mechi hiyo iliyopigwa juzi, mabao ya KVZ yalipachikwa kimyani na Suleiman Abdi dakika ya tisa, Said Salim dakika ya 67 na 72 huku bao pekee la kufutia machozi kwa timu ya Tekeleza likiwekwa kimiani na Ali Mohamed Ngwali dakika ya 86.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo kumalizika, Kocha wa KVZ, Sheha Khamis, alisema haikuwa kazi rahisi kufanikisha lengo lao la kuunyakuwa ubingwa wa FA baada ya kuukosa ule wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Alisema wachezaji walijituma na walionyesha moyo wa dhati wa kuhakikisha timu hiyo inafanikiwa kuchukua kombe hilo kwa kucheza kwa hamasa kwa kuzingatia maelekezo yake.

Khamis alisema kwa sasa wanapaswa kuanza maandalizi mapema ikiwamo ya Ligi Kuu Zanzibar msimu mpya pamoja na kombe hilo la shirikisho ili kufanikisha lengo lao la kufanya vizuri katika michuano hiyo mikubwa.

"Kwa dhati niwapongeze wachezaji pamoja na viongozi wa KVZ, wamefanya kazi nzuri, wamejituma kuhakikisha lengo letu linatimia, ilikuwa michuano migumu kwa kuwa timu zilizokuwa zinashiriki ikiwamo zile za kutoka madaraja ya chini, ni timu ambazo zilikuwa na wachezaji wazuri na wenye uwezo, lakini Alhamdulilah sisi tumefanikiwa kuvuka hatua zote," alisema.

Kocha huyo aliwapongeza pia mashabiki wa KVZ ambao mara nyingi wamekuwa wakijitokeza uwanjani kutoa hamasa pale timu yao inapokuwa ikicheza.

# Michezo

Jumatatu Agosti 24, 2020

Nipashe




Ronaldo kwa Mbappe, amkataa Neymar Real UKURASA 22

ZAMU YENU...



Mshambuliaji wa Simba, Mghana Bernard Morrison (mbele), akishangilia na Said Ndemla, baada ya kuifungia timu yake bao la kuongoza dhidi ya Vital'O ya Burundi katika Uwanja wa Mkapa juzi. Staili hiyo aliitumia kushangilia wakati alipoifunga Simba akiwa Yanga. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BWALYA, ONYANGO GUMZO SIMBA DAY

## ●●● Waanza kuwafunga midomo wanaobeza usajili Simba, Sven akunwa na majembe, asema...

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa Simba wamekoshwa na uwezo ulioonyeshwa na wachezaji wao wapya waliosajiliwa katika dirisha hili la usajili, baada ya kuwashuhudia wakionyesha viwango vya kuridhisha katika mechi yao ya kwanza kuichezea klabu hiyo kwenye Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam juzi.

**Katika mchezo huo wa kirafiki dhidi ya Vital'O ya Burundi, ambao Simba ilishinda mabao 6-0, iliwachezesha nyota wote waliosajiliwa msimu huu, lakini walioonekana kuwakuna zaidi mashabiki ni kiungo Mzambia Larry Bwalya na beki wa kati, Mkenya Joash Onyango.**

Akicheza nafasi ya beki wa kati sambamba na Ibrahim Ame aliyesajiliwa dirisha hili akitokea Coastal Union ya Tanga, Onyango alionyesha ubora zaidi upande wa kushoto huku Ame naye akifanya vizuri kulia, jambo ambalo mashabiki wa Simba walionekana kufurahishwa nalo wakati huu ikiwa ndiyo kwanza wawili hao kucheza pamoja.

Mara baada ya kutua nchini, mashabiki wengi walimbeza Onyango wakiitania Simba imesajili 'babu' kwa kile walichodai umri unaonekana kumtupa mkono na haendani na miaka 27 anayoeleza ndio umri wake kwa sasa.

Lakini Onyango alisema: "Nimekuja kufanya kazi Simba, wale wanaojadili umri wangu kwa sasa, watakuja kunyamaza na watajutia kauli zao, kwa kazi nitakayoonyesha uwanjani."

Hata hivyo, kwa mechi yake ya kwanza tu tena kwa dakika 45 alizocheza mashabiki walianza kumkubali, wakisema: "Jamaa anajua, angalia alivyotulia na wanaelewana na Ame kama wamecheza naye miaka mingi, hapa tumepata beki," vikundi vya mashabiki wa Simba wakati wa mapumziko walisikika wakimjadili.

Lakini pia, Bwalya naye alionekana kuwa kivutio kikubwa katika mchezo huo, na mashabiki hawakusita kueleza ni mchezaji ambaye atatoa ushindani mkubwa katika nafasi ya kiungo dhidi ya Mzambia mwenzake, Clatous Chama.

"Kazi ipo kwa Chama na viungo wenzake, huyu Bwalya ana jicho la pasi, angalia namna anavyomiliki mpira na kugawa, hasa alivyomchungulia Bernard Morrison na kumdondoshea akafunga," alisema shabiki aliyejitambulisha kwa Juma Abdallah wakati wakimjadili kiungo huyo.

Katika mchezo huo, ambao ulikuwa maalum kwa ajili ya kuhitimisha kilele cha Wiki ya Simba maarufu Simba Day, washambuliaji wote wapya wa Simba, Bernard Morrison, Chris Mugalu na Charles Ilamfya walicheka na nyavu, lakini jicho la mashabiki lilielekezwa zaidi kwa Onyango na Bwalya.

Simba ilianza kupata bao la kwanza dakika ya 42 kupitia kwa Morrison akipokea pasi ndefu kutoka kwa Bwalya huku dakika tatu baadaye nahodha John Bocco akifunga baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Morrison aliyemzidi ujanja mlinzi wa Vital'O, hivyo kwenda mapumziko wakiongoza 2-0.

Kipindi cha pili Simba ilibadili kikosi chote ambacho kilianza, na Chama kuifungia bao la tatu dakika ya 57 baada ya kupokea mpira mrefu kutoka katikati ya uwanja uliopigwa na Ibrahim Ajibu. Baada ya kazi hiyo nzuri, Ajibu aliziona nyavu mwenyewe dakika ya 77 akipokea mpira uliobetuliwa juu na Chama, hilo likiwa ni bao la nne.

Dakika mbili baadaye usajili mpya, Mugalu aliipatia bao la tano kwa shuti kali ndani ya 18 akipokea pasi safi kutoka kwa Miraji Athumani upande wa kushoto kabla ya

Ilamfya kukamilisha karamu hiyo ya mabao kwa kufunga bao la sita dakika ya 92 akimalizia mpira wa krosi uliopigwa na Mohammed Hussein 'Tshabalala'.

Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck akizungumzia kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake alisema: "Mechi ilikuwa ngumu na nzuri, wachezaji wote wamefanya kile nilichowaelekeza mazoezini, hili jambo zuri na linanipa matumaini ya kufanya vizuri huko mbeleni.

"Safu ya ushambuliaji ipo vizuri, nina uhakika wa kumpanga mtu, endapo kutakuwa na mgonjwa au kutumikia adhabu, sitapata wakati mgumu."

# Morrison aiamsha Yanga, agandwa

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuanza kuonyesha uwezo kwa kuifungia Simba bao kwenye mechi yake ya kwanza na kutoa pasi moja ya mwisho, huku akiisifu klabu hiyo ni bora kwake na ni sawa na chuo kikuu cha soka, Yanga imesema sakata lake bado ni bichi na inamtambua ni mchezaji wao halali.

Juzi Morrison alionyesha kiwango cha juu akichezea Simba dhidi ya Vital'O katika Uwanja wa Taifa wakati ikishinda 6-0 kwenye mechi ya kuhitimisha kilele cha Wiki ya Simba, maarufu Simba Day na wakati akitambulishwa nyota huyo raia wa Ghana alisema anaipenda sana klabu hiyo na kwa hapa nchini ni kama chuo kikuu cha soka.

Lakini Mwenyekiti wa Klabu Yanga, Dk. Mshindo Msolla, akiwa jijini Dodoma juzi wakati wakiendelea na madhimisho ya kuelekea kilele cha Siku ya Mwananchi Agosti 30, mwaka huu, alisema hawatosimama hadi haki yao ipatikane kuhusu Morrison.

"Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji walisema kuwa kulikuwa na mapungufu kwenye mkataba. Kuwa na mapungufu kwenye mkataba hakuwezi kuhalalisha kusema kuwa hakukuwa na mkataba. Kwa hiyo sisi tumemwordhesha kama mchezaji wetu, tunapeleka usajili wake, lakini pia tunatuma kwenye mtandao wa TMS na Jumatatu (leo) tunapeleka mashtaka au rufani yetu Shirikisho la Soka Duniani (FIFA).

"Wakisema ni mchezaji wetu, basi Simba waje kama wanamhitaji, lakini si kumchukua kwa staili hii, sisi hatumgombei, ila ni taratibu tu zifuatwe," alisema.

Hivi karibuni, Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF ilimpa ushindi Morrison katika kesi ya kutokuwa na mkataba na Yanga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >